# TATHMINI YA MATUMIZI YA VIFAA VYA KUFUNDISHIA MSAMIATI WA KISWAHILI KATIKA SHULE ZAMSINGI ZA UMMA, KAUNTI YA KISUMU MASHARIKI, KENYA

NA

KAMAU HELLEN WAMBUI

TASNIFU IMETOLEWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA TAALUMA YA ELIMU NA UFUNDISHAJI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SEPTEMBA, 2015

ii

**UNGAMO NA IDHINI**

Utafiti huu ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine.

SAHIHI: ............................................ TAREHE: 2/11/2015

KAMAU HELLEN WAMBUI

E55/CE/23565/2011

Ripoti hii ya utafiti imetolewa Kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

SAHIHI: ............................................ TAREHE: 3/11/15

DAKTARI BABUSA HAMISI

IDARA YA TEKNOLOJIA NA MAWASILIANO

SAHIHI: ............................................ TAREHE: 03/11/15

DAKTARI SAMSON ONDIGI

IDARA YA TEKNOLOJIA NA MAWASILIANO

# TABARUKU

Naitarabuku kazi hii kwa mwanangu wa pili, marehemu Simon Kanyora.Kupitia kwake,nilipata motisha wa kuendeleza masomo yangu kwa bidii na subira. Rabukaamrehemu.

## SHUKRANI

Kazi hii, ingawa nimeifanya, imechangiwa na watu mbalimbali. Ni kweli kuwa kidole kimoja hakivunji chawa. Kwanza, namshukuru Mungu kwa kunipa pumzi, siha mwilini na hekima iliyoniongoza, tokea awali, nilipoanza kujitosa katika uwanja huu wa usomi. Ameniongoza katika safari hii ndefu iliyojaa kila aina ya pingamizi na kunifikisha umbali huu wa kuitimiza ndoto yangu ya miaka mingi ya kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili. Nimekosa neno halisia la kutosheleza shukrani ninazoshenezea Mwenyezi Mungu maishani.

Shukrani nazitoa kwa wasimamizi wangu: Daktari Hamisi Babusa na Daktari Samson Ondigi, kwa mwelekeo waliyonipa katika utafiti wangu, na kwa subira ya hali ya juu waliyoonyesha, hasa pale nilipoonekana kukosa mwelekeo niliyazingatia maelekezi yao, ambayo kwa hakika, ndiyo sababu hasa ya ufanisi wa kazi hii.

Mgao mwingine wa shukrani umwendee MC Onyango wa Chuo Kikuu cha Maseno walioniangazia katika njia zote nilizozipitia. Vilevile namshukuru mwalimu John Kapufi, John Mwaura na Dominic Deka waliopata nafasi ya kukagua kazi yangu, kunikosoa, kunihimiza na kuendelea mbele. Haiwezekani kuwasahau wanafunzi wenzangu tulioabirimimi pamoja mtumbwi huu wa usomi. Ni vizuri kuwa sote tumekuwa tukisaidiana kuendeleza masomo yetu hadi sasa.

Ningependa kuwashukuru walimu wenzangu wa shule ya Msingi ya Aga Khan, Kisumu walionisaidia kupata wakati wa kuboresha kazi yangu. Namshukuru mamangu kwa maombi aliyotoa wakati wa mitihani na safari zangu chuoni. Wanangu Tony Kamau na Jeff Kanyora kwa motisha na changamoto walizonipa kuendeleza masomo yangu, mume wangu Benson Kamau Kanyora ambaye alijitolea kwa hali na mali kuhakikisha kwamba yote yaliendelea bila utata wowote. Mwisho nawashukuru wapiga taipu: Elizabeth Mwangi na Kiptala wa Idara ya Teknolojia walio nisaidia katika kazi hii. Kwenu nyote mlioshiriki katika kurahisisha kazi hii nasema asanteni na Mungu awape thawabu.

# YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ...................................................... Error! Bookmark not defined.

TABARUKU ........................................................................................................ iii

SHUKRANI ........................................................................................................ iii

YALIYOMO ........................................................................................................ iv

ORODHA YA MAJEDWALI ................................................................................. v

ORODHA YA MICHORO .................................................................................... vi

FASILI YA UFUPISHO ....................................................................................... vii

IKISIRI…... ...................................................................................................... viii

Sura Ya Kwanza: Utangulizi ................................................................................ 1

1.1 Usuli Wa Utafiti ........................................................................................ 1

1.2 Suala La Utafiti .......................................................................................... 3

1.3 Malengo Ya Utafiti ..................................................................................... 4

1.4 Maswali Ya Utafiti ..................................................................................... 4

1.5 Sababu Za Kuchagua Mada ......................................................................... 4

1.6 Umuhimu Wa Kushughulikia Utafiti Huu ..................................................... 7

1.7 Upeo Na Mipaka Ya Utafiti .......................................................................... 7

1.8 Upungufu Wa Utafiti Huu ............................................................................ 7

1.9 Kiunzi Cha Dhana ........................................................................................ 8

1.9.1 Mgofu Huu Unaonyesha Matokeo Bora Ya Mtihani Yatapatikana Ikiwa :......... 8

1.9.2 Hitimisho Ya Kiuzi Cha Dhana .................................................................. 8

1.10 Nadharia Ya Utabia ..................................................................................... 9

1.11 Mgofu Wa Utafiti ........................................................................................ 10

Sura Ya Pili: Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ......................................................... 13

2.1 Changamoto Za Kutumia Visidizi Vya Ufundishaji .................................... 13
2.2 Sera Za Ukanguzi Matumizi Ya Visaidizi Vya Ufundishaji ........................... 15
2.3 Udhaifu Na Ufaafu Wa Matumizi Ya Visaidizi Vya Ufundihsaji ................... 17
2.4 Hitimisho Yalioandikwa Kuhusu Mada ..................................................... 23

**Sura Ya Tatu: Mbinu Za Utafiti..........................................................................24**

3.1 Mbinu Za Utafiti.......................................................................................... 24
3.1.1 Hitimisho La Kiunzi Cha Dhana ................................................................ 25
3.2 Eneo La Utafiti ............................................................................................ 25
3.3 Walengwa.................................................................................................... 25
3.4 Uteuzi Wa Sampuli...................................................................................... 26
3.5 Visaidizi Vya Utafiti ................................................................................... 27
3.5.1 Hoja..I.........................................................................................................27
3.5.2 Nakala Ya Uchunguzi ..................................................................................27
3.6 Idadi Ya Walengwa ..................................................................................... 28
3.6.1 Utafiti Wa Awali ......................................................................................... 28
3.7 Ukusanyaji Wa Data ................................................................................... 29
3.7.1 Hojaji........................................................................................................... 29
3. 7.2 Nakala Ya Uchunguzi................................................................................. 29
3.7.3 Mahojiano.....................................................................................................30
3.8 Uchanganuzi Wa Data ................................................................................. 30
3.9 Udhabiti Wa Visaidizi.................................................................................. 30
3.10 Uthamini ..................................................................................................... 30
3.11 Usiri ............................................................................................................. 31

**Sura Ya Nne: Uchanganuzi Wa Data ......................................................................32**

4.1 Habari Za Kibinafsi Kuhusu Wahojiwa.................................................................32

4.2 Changamoto Zilizopo.............................................................................................34

4.3 Sera Za Kudhibiti Matumizi Mwafaka Ya Visaidizi...................................... 42

4.4 Udhaifu Au Ufaafu Wa Matumizi Ya Visaidizi Vya Ufundishaji .................. 45

Sura Ya Tano: Muhtasari, Hitimisho Na Mapendekezo ..............................................**49**

5.1 Utangulizi ..............................................................................................**49**

5.2 Muhtasari ..............................................................................................**49**

5.3 Hitimisho ..............................................................................................**49**

5.4 Mapendekezo..........................................................................................**50**

5.4.1 Mapendekezo Ya Utafiti......................................................................**51**

5.4.2 Mapendekezo Yanayo Zingatia Utafiti Zaidi.......................................**51**

Marejeleo ....................................................................................................**52**

**Orodha Ya Viambatisho**

Kiambatisho 1: Hojaji za walimu wakuu........................................................................ 56
Kiambatisho 2:Hojaji za walimu wakuu.......................................................................... 65
**Kiambatisho 3: Hojaji ya Wanafunzi** ........................................................................ 73
Kiambatisho 4:Nakala za mtafiti kuchunguza somo ...................................................... 78
Kiambatisho 5: Nakala ya uchunguzaji wa somo la Kiswahili....................................... 79
Kiambatisho 6: Cheti cha Idhini ya NACOSTI ............................................................... 81
Kiambatisho 7: Barua ya idhini NACOSTI...................................................................... 83
Kiambatisho 8: Kibali cha Utafiti .................................................................................... 84

## ORODHA YA VIFUPISHO NA UFAFANUZI WA DHANA

| | |
|---|---|
| CLT | Communicative Language Teaching (Kufunza lugha kwa mawasiliano) |
| KNEC | Kenya National Examination Council (Baraza la Mitihani Nchini Kenya) |
| MOEST | Ministry of Education Science and Technology (Wizara ya Elimu Sayansi na Teknologia) |
| PDSI | Plan, Do, See, Improve (Kupanga, kufanya, kuona na Kuimarisha) |
| UNESCO | United Nations Educational Scienfitic Education Organization (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Sayansi) |

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Linganisho la matokeo ya Kiswahili katika KCPE na Darasa la 3 .......................................... 3

Jedwali 2: Idadi Ya Wanafunzi wa Kiswahili ................................................................................ 26

Jedwali 3: Idadi Ya Walimu Wa Kiswahili .................................................................................. 27

Jedwali 4: Kidhibiti Cha Walimu Wa Kiswahili Katika Kila Shule ........................................................ 28

Jedwali 5: Kiwango cha matumizi ya visaidizi vya ufundishaji na walimu shuleni .................................. 35

Jedwali 6: Matumizi ya visaidizi madarasani .............................................................................. 37

Jedwali 7: Kiwango cha mwalimu wa Kiswahili anachotumia visaidizi ................................................ 37

Jedwali 8: Maoni kuhusu umuhimu utumiaji visaidizi vya ufundishaji ................................................ 39

Jedwali 9: Sera ya kudhibiti matumizi mwafaka ya visaidizi madarasani ............................................. 42

Jedwali 10: Wenye uamuzi kuhusu ununuzi…………………………………………………………….. 50

Jedwali 11: Jinsi visaidizi vya ufundishaji vinavyochangia……………………………..……………..51

# ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1: Kiunzi cha dhana ........................................ 13

Mchoro 3: Jinsia ya Walimu Wakuu ........................................ 35

Mchoro 4: Viwango vya elimu ya walimu wa Kiswahili ........................................ 36

Mchoro 5: Kiwango cha matumizi ya visaidizi vya ufundishaji na walimu shuleni ........................................ 38

# ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Hojaji za walimu wakuu .................................................... **Error! Bookmark not defined.**

Kiambatisho 2:Hojaji za walimu wakuu ..................................................... **Error! Bookmark not defined.**

Kiambatisho 3:Hojaji ya wanafunzi............................................................ **Error! Bookmark not defined.**

Kiambatisho 4:Nakala za mtafiti kuchunguza somo................................... **Error! Bookmark not defined.**

Kiambatisho 5: Nakala ya uchunguzaji wa somo la Kiswahili................... **Error! Bookmark not defined.**

Kiambatisho 6: Cheti cha Idhini ya NACOSTI .......................................... **Error! Bookmark not defined.**

Kiambatisho 7: Barua ya idhini NACOSTI ................................................ **Error! Bookmark not defined.**

Kiambatisho 8: Kibali cha Utafiti ............................................................... **Error! Bookmark not defined.**

## IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia uchunguzi wa matumizi ya vifaa vya ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili katika shule za msingi za umma, Kaunti Ndogo ya Kisumu Mashariki, Kenya. Madhumuni aliyozingatia mtafiti katika utafiti huu yalikuwa ni pamoja na kutambua changamoto zilizopo wakati wa kutumia vinyago, video na chati katika somo la msamiati, pili ni kudadisi sera zilizopo za ukaguzi ili kudhibiti matumizi wa video, chati na vinyago ili kusaidia uelewekaji wa misamiati na kuchunguza udhaifu na ufaafu uliopo katika ufundishaji msamiati kwa kutumia video, chati na vinyago katika somo la Kiswahili.Utafiti ulifanywa katika shule kumi za Kisumu Mashariki. Hojaji zilitumika kukusanya data ya walimu mkuu, walimu wa Kiswahili.Nakala ya uchunguzi somo ya walimu wa Kiswahili ilitumika .Uteuzi wa sampuli ya wanafunzi ,walimu wa Kiswahili ilikuwa ya unasibu na sampuli kusudi kwani walengwa hawa ndio walikuwa na vigeu ambavyo mtafiti alihitaji.Data ilikusanywa kwa vifaa hivi vya utafiti,nakala ya uchunguzi na hojaji.Utafiti awali ulifanyika ili udhabiti na uthamni upatikane kabla utafiti halisi, ili kurekebisha kasoro .Mbinu iliyotumika ya kushughulikia utafiti ni kwanza kuteua kichwa,uteuzi wa shule husika ,walengwa wa utafiti ,njia za kukusanya data,kuchanganua data,,kudhibiti na kudhamni vifaa ili kurekebisha makosa kabla ya utafito wenyewe. Utafiti ulidhibitisha somo lenye vifaa hufurahiwa,huvutia hisia ,hurahisisha uelewa wa dhana, hivyo kuboresha matokeo ya mtihani.Utafiti ulilenga idadi ya walimu kumi wa Kiswahili katika Shule za msingi katika Kaunti ya Kisumu Mashariki.Mtafiti aliteua sampuli kwa bahati nasibu. Walengwa walioteuliwa walikuwa walimu wakuu kumi, walimu wa Kiswahili kumi na wanafunzi kumi. Walengwa wote walikuwa mia nane ishirini ambao walikuwa asilimia kumi, basi idadi iliyohojiwa ikawa themanini na mbili . Hojaji zilikuwa aina tatu: za walimu wakuu, walimu wa Kiswahili na wanafunzi. Utafiti ulichanganulia kwa kutumia kifaa cha uchanganuzi data( SPSS) kuonyesha idadi katika alama za asilimia na uradidi. Baada ya kutafiti na kuchanganua data, mtafiti alipendekeza kuwa, kuna haja ya walimu wa Kiswahili kuwa na vikao katika majopoili wajadiliane na kutayarisha visaidizi wanavyohitaji ili kuboresha ufunzaji na uelewekaji wa msamiati. Pamoja na hayo,walimu wanahitaji kuunda sera za kutengeneza visaidizi vya somo la Kiswahili zitakazowawezesha kupanga mikakati ya kukaguana wao kwa wao. Jambo hili litakuza umoja wa kufaana. Mtafiti pia alionelea kuwa kuna haja ya washika dau wote wa elimu kufufua taasisi za Kaunti ili kukuza hitaji la uundaji visaidizi ili walimu waendeleze weledi wao wa kuunda visaidizi ili kuboresha uelewekaji wa dhana za Kiswahili. Kadhalika,washika dau wana changamoto kubwa ya kuleta mashuleni rasilimali za kutosha kutengeneza visaidizi vinavyohitajika. Jambo lingine ni kuwa shulezitengesehemu mahususi za kuhifadhi visaidizi ili vitumike bila uwoga wa kuharibika ama kupotea. Mwisho, walimu waweke misingi thabiti ya ufunzaji msamiati kuanzia madarasa ya chini ili wanafunzi wazielewe dhana hizi kimakosa, kisha pawe na hitaji kuzirekebisha baadaye.

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1 Usuli Wa Utafiti

Leo hii ulimwengu unapitia mabadiliko ya haraka, hivi kwamba mbinu za ufunzaji za kimapokeo zimebadilishwa na dhana mpya za elimu. Ndiposa elimu ya kipindi hiki, imetoa mwito katika karne hii kuliko ilivyokuwa hapo awali. Ulimwengu uko ukingoni mwa awamu ya kusisimua na ya kimapinduzi, ambayo uchunguzi wa kisayansi wa binadamu utaboreshwa kwa masilahi yake wenyewe. Elimu sharti itekeleze wajibu wake. Baraza la elimu wanakiri kuwa mageuzi katika utendaji katika elimu yanawezekana na hayaepukiki. Mahitaji mapya na maono mapya yanahitajika katika elimu kwa namna ambayo yanaleta kiwango cha ubora ambao haukuwahi kutazamiwa katika historia ya mwanadamu. Quist (2005) aliwahi kudai kuwa “Elimu hii mpya ni falsafa ya kielimu inayoboresha utendaji kazi katika shule, kufanya mafunzo kuwa na nguvu, kuwapa watoto hisi ya uhalisia shuleni, kufanya shule ziwe maabara, karakana, maktaba na majaribio ya kuzinduka kwa elimu”

Nunan: (2009) asemaye,misingi ya ki-elimu ya kiasili, kisosiolojia, kifisiolojia na kifalsafa, kumeibuka miondoko muhimu katika utendaji wa kufunza na kujifunza. Kufunza kuzuri ni kule kunakosababisha, kusuluhisha na kukuza ujifunzaji. Ili kufanikisha lengo hili, mwalimu, kama wafanyavyo mafundi wengine, sharti atumie mbinu maarufu kama zile zinazohusisha visaidizi vya kufunzia. Visaidizi hivi ni maumbo mbalimbali yanayodhihirika mara kwa mara. Ingawa visaidizi vya kufunzia hutumika katika masomo, baadhiya vifaa hupotosha, huleta fikira potovu inayotokanana kutokuwepo kwa makini na matumizi yanayofaa kiwakati. Utafiti huu ulinuiakutathmini jinsi matumizi ya visaidizi katika kufunza msamiati huboresha uelewa katika shule za msingi za umma katika wilaya ya Kisumu Mashariki,nchini Kenya. Shabaha ya utafiti huu ni kudhihirisha sababu za kutotumia visaidizi hivyo kwa makini, kutambua vikwazo vya matumizi ya visaidizi na kutoa ushahidi wa jinsi visaidizi vya kufunzia vinavyofanikisha uelewa wa dhana zilizofunzwa.

Utafiti huu ulitumia kiunzi cha kinadharia cha John Dewey kinachosisitiza uasilia na vipengele vyake muhimu. Wazo hili pia linashikiliwana Piaget (1945) huku akimunukuu

John Dewey kama mwanadhana shupavu katika mwanzo wa miaka ya 1900.Alisema kwamba mchezo ni jambo fiche ambalo husaidia mtu pekee kukua kisosiolojia na kiakili. Jambo hili lazima litengwe na kazi kwani mchezo husaidia mtoto kukua kama mtu mwenye ari ya kufanya kazi. Watoto wanapokuwa watu wazima huacha mchezo na kutafuta motisha katika kazi zao. Jambo hili la kazi za mchezo humtayarisha kuwa mtu mzima aliye na afya na ari ya kazi. Uteuzi wa kusudi na sampuli ilitumiwa kuchagua matumizi makinifu ya visaidizi vya kufunzia. Tomlinson (2012) anaeleza kuwa data ilikusanywa kwa njia ya mahojiano na kuchanganuliwa kwa kuzingatia ubora wake. Mtafiti alitumaini kuwa utafiti huu ungenufaisha shule za umma, Kisumu Mashariki, idara ya elimu, kaunti ya Kisumu mashariki,wanafunzi na walimu ili kudhibiti matumizi mabovu ya visaidizi, kutoeleweka vizuri kwa msamiati na matokeo duni ya wanafunzi. Kujifunza hutokana na mwingiliano kati ya mwalimu, wanafunzi, wazazi na jamii kwa jumla. Matokeo ya ujifunzaji hujitokeza katika mpangilio wa kujifunza unapobuniwa. Matokeo haya hutegemea pakubwa mpangilio uliopo wa shule katika ujifunzaji. Uelewekaji wa msamiati hutegemea visaidizi vya ujifunzaji vinavyotumika kurahisisha somo Brown, Oke & Brown: (2006).

Uchangamuzi wa data ya mtihani wa kitaifa wa mjini Kisumu mwaka wa 2011,ulionyesha shule 47 katika ya shule 118 zilipata chini ya alama 250 kwa alama 500 ambapo ni asilimia arubaini (40%) ya jumla ya shule zote na alama asilimia hamsini (50%) ya nambari yote husika. Mwaka wa 2010, shule 48 hazikupata alama 250 asilimia arubainina moja (41%) ya shule zote. Kulingana na afisi kuu ya washika dau wa elimu Kisumu Mashariki (Kisumu Municipal Education Office Performance Report mwaka 2011) shule tano za chini zilipata alama ya wastani 175.29, 186.37, 190.28, 194.01 na 191.86. Uchanganuzi huu unadhihirisha kuwa alama duni katika matokeo ya mtihani wa kitaifa katika shule za umma katika Manispaa ya Kisumu, Kutoka (2013, Januari 29), mwaka 2012, data ya matokeo ya shule tano zilizokuwa za mwisho Magharibi, Kaunti ya Kisumu, na kaunti majirani zilipata alama 162.8, 176.8, 197.0, 190.2 na 174.8. Hii ni kwa sababu ya kutotumia mbinu mwafaka na visaidizi vya ufundishaji msamiati. Kutokana na data hii basi ni bayana kwamba kulikuwa na haja ya utafiti ambao utaeleza umuhimu wa visaidizi vya kufundishia. Utafiti huu ulilenga kutambua umuhimu wa matumizi ya

visaidizi vya kufunza msamiati ili kuboresha uelewekaji msamiati katika shule za umma za Kaunti ya Kisumu. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mitihani ya darasa la tatu ya miaka miwili kuthibitisha kwamba kuna pengo linalohitaji kuzibwa. Matokeo ya Kiswahili vile vile katika darasa la nane kutoka shule hizo hizo yalikuwa alama za chini hivyo kutaka kuziba pengo la matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa.

**Jedwali 1: Linganisho la matokeo ya Kiswahili katika KCPE na Darasa la 3**

| SHULE | 2011 | | 2012 | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | KCPE | STD 3 | KCPE | STD 3 | |
| A | 71.05 | 71.35 | 65.65 | 67.43 | 130 |
| B | 54.09 | 58.80 | 55.70 | 57.18 | 172 |
| C | 58.15 | 42.63 | 62.04 | 39.41 | 114 |
| D | 57.67 | 69.3 | 56.59 | 68.38 | 85 |
| E | 57.32 | 43.25 | 65.76 | 50.3 | 94 |
| F | 53.46 | 59.61 | 53.61 | 54.54 | 24 |
| G | 59.65 | 59.65 | 60.33 | 60.51 | 105 |
| H | 60.39 | 44.30 | 52.26 | 31.47 | 76 |
| I | 53.46 | 58.80 | 58.51 | 57.18 | 86 |
| J | 39.67 | 57.5 | 44.86 | 61.80 | 39 |

(Afisi kuu ya washika dau elimu Kaunti ya Kisumu)

## 1.2 Suala La Utafiti

Visaidizi vina dhima kuu ya kutekeleza katika ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Inadhihirisha kuwa walimu wengi wanafunza Kiswahili vibaya. Hawafanyi juhudi kuwaonyesha wanafunzi na kuwathibitishia wanachofunza. Hii huenda ikasababishwa na kutoelewa umuhimu wa matumizi ya visaidizi katika kufundisha msamiati. Kulingana na Kathleen (2012), ni vyema kufahamu kuwa visaidizi vikiwepo na havitumiki si sawa. Ni muhimu visaidizi vitumike ifaavyo. Walimu wanahitaji kuchukua muda katika utengenezaji na utayarishaji wa visaidizi. Changamoto za walimu huwa kuvipata visaidizi hivyo na ueledi wa kuvitengeza Ukiwa mwalimu mfawidhi, ni jukumu lako kuratibu utengenezaji na uratibu wa visaidizi ili kukidhi mahitaji ya walimu pamoja na wanafunzi. Wasemavyo Mogeni, Kathleen, Pretorius,Allinder visaidizi vya kufundisha vina dhima kubwa,changamoto za kuhifadhi hivyo vifaa ni tele na jinsi ya kupata rasmali ya kununua vifaa hivyo,lakini tafauti zilizopo na utafiti wangu ni upeo, njia ya kukusanya data,uchanganuzi wa data, walengwa,njia za uteuzi wa sampuli,aina za vifaa na mapendekezo waliopendekezo . Hivyo kuzua pengo hili la kutathmini matumizi ya vifaa

vya kufundisha msamiati wa Kiswahili katika shule za msingi,katika kaunti ya Kisumu mashariki,Kenya ili kuboresha matokeo ya Kiswahili.

### 1.3 Malengo Ya Utafiti

(1) Kubainisha changamoto zilizopo katika kutumia vinyago, video na chati katika somo la msamiati wa Kiswahili.

(2) Kufafanua sera zilizopo za ukaguzi, matumizi ya visaidizi katika kufunza msamiati wa Kiswahili.

(3) Kueleza udhaifu na ufaafu uliopo katika ufundishaji msamiati kwa kutumia video, chati na vinyago katika somo la Kiswahili.

### 1.4 Maswali Ya Utafiti

(1) Je, ni changamoto zipi zilizopo wakati wa kutumia vinyago, video na chati katika somo la msamiati?

(2) Ni sera zipi za ukaguzi wa somo hutumika katika kufundisha msamiatizikitumia visaidizi mwafaka?

(3) Ni nini udhaifu na ufaafu wa matumizi ya vinyago, video na chati katika somo la Kiswahili?

### 1.5 Sababu Za Kuchagua Mada

Watafiti kama Mogeni (2005),Kathleen(2012),Patel & Mukwa (1993) na wengine wanatambua kwamba utumiaji wa visaidizi huteka makini ya wanafunzi, kuwatia hamu na ari ya kujifunza, kuchochea ubunifu wa wanafunzi, kurahisisha maelezo ya maneno, kutoa muhtasari wa yaliyofunzwa na kuzindua utaalamu wa wanafunzi. Wanafunzi hukumbuka vizuri wanachokiona na kutenda kuliko wanachokisikia mara nyingi walimu.Kwa Mfano:Katikakufundisha msamiati wa vyakula na kueleza tofauti ya pilipili mboga na pilipili hoho, hadi leo ni tatizo sugu.Wanafunzi wengi bado wanasema kinyume; pojo huitwa ndengu na ndengu huitwa pojo. Katika msamiati wa mavazi;

kaptula, chupi na suruali, yote ni mamoja na hawajui kwamba ni tofauti, kofia na chepeo huwa pia hubainisha tofauti.

Matumizi ya visaidizi kiholela bila kuzingatia wakati unaofaa husababisha wanafunzi kutoelewa vyema.Watajishughulisha zaidi kutazama visaidizi ulivyoviandaa kuliko yaliyomo katika funzo. Mpango wa wakati wa kutumia visaidizi kwa uangalifu kurekebisha matatizo haya. Baadhi ya walimu huchukulia visaidizi vya ufunzaji kuwa vinawapunguzia ugumu wa maisha yao kazini. Hivyo basi wanavunjika moyo kwa urahisi mara tu wanapogundua kuwa pana ugumu wa kuvitengeneza na kutayarisha matumizi yavyo. Visaidizi huwa na matumizi mbalimbali wakati wa kuendeleza somo. Kwanza, inafaa kufahamika kwamba visaidizi hivi si mbinu kamilifu ya kufundisha bali husaidia kufaulisha somo. Pili, ni muhimu kutambua umuhimu wa matumizi ya visaidizi katika somo. Uteuzi wa visaidizi mwafaka katika somo ni muhimu. Vigezo vya kuzingatiawakati wa uteuzi wa visaidizi ni pamoja na ufaafu wa visaidizi, utayarishaji wa visaidizi na kuafiki kwa visaidizi. Vinginevyo ni pamoja na matumizi ya visaidizi kwa wakati ufaao, ubora wa visaidizi, ukubwa wa idadi yake na hali ya visaidizi.

Su na Hong (2007) wana msimamo kwamba walimu lazima wawe na ujuzi maalumu kuhusu wanafunzi katika mambo na kazi fulani na jinsi ya kupokeza na kufunza dhana hizo. Naye Riley (2005) anasema kwamba kufunza ni tendo la kuwasilishwa kwa hali ya jambo halisia au lisilo halisia. Kwa hivyo tunapofunza ni lazima au ni vyema kujua wanafunzi na somo. Kadhalika, Wang (2009) anatambua kuwa ni vyema vilevile kujua jinsi ya kufunza kwa ujumla na hasa katika hali halisia na vipaji halisia vipasavyo katika hali hiyo au kwa dhana hiyo. Kule kubadilika kwa majukumu fulani kunamaanisha kwamba mwelekezi lazima aonyeshe ustadi wa vipaji fulani kuliko mwalimu.Alinder (2001) anasema mwalimu hunena, mwelekezi huuliza, mwalimu huzungumza kutoka mbele, mwelekezi huelekeza na kutoa mwelekeo na kuibua mazingira mwafaka kumwezesha mwanafunzi kubuni maoni yake mwenyewe. Mwalimu huzungumza lakini mwelekezi huzua majadiliano na wanafunzi Wolfenson (2000). Mwelekezi lazima awe na uwezo wa kujadili na kupokea ujifunzaji mpya kwa kufululiza mawazo mapya hadi palewanafunzi wabunipo jambo jipya au kutoa maoni yao.

Mazingira ya ujifunzaji lazima yawe ya kusaidia na kutoa changamoto za kufanya wanafunzi wawe wa kutumia bongo vizuri Wringe (2000). Kule kuwatetea wanafunzi kuwa wenyeji wa shida na usuluhishaji kazi, si kwamba kila zoezi au suluhisho limetosheleka. Mwalimu awe mwelekezi na wanafunzi watenda kazi. Wananadharia ya ki-Vygostki wanasisitiza kwamba watoto wanaohitaji kufanya kazi au zoezi ambalo watafaulu kwa usaidizi unaotolewa. Wanasisitiza kwamba mtoto anahitaji ambalo lazima litambuliwe na kukuzwa iwapo matumizi ya visaidizi yatatiliwa maanani.

Hali na zoezi ni muhimu na lazima katika ujifunzaji dhana. Kwa hivyo, mwanafunzi lazima afanye zoezi halisi kila siku kwa sababu ya kuzua maana na hitaji kwa kunukuu Just & Carpenter (2002). Ili dhana ieleweke, mwelekezi atatoa zoezi la wanafunzi ambapo watafanya pamoja. Huku kutawafanya kutumia vipawa vyao na kupata mwingiliano ambao utasaidia kurahisisha uelewa wa dhana za taaluma mbalimbali. Watafiti hao wanasema kwamba hayo yote yatafanyika mwalimu anapotayarisha visaidizi vya kujifunza na kutengeneza mazingira mwafaka ili kazi hii iwezekane na wanafunzi wenye tofauti hizo watajifunza kwa urahisi, kutazama na kukumbuka dhana zilizofunzwa kwa urahisi.

Ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za msingi una utata mwingi. Kwanza kabisa, walimu wenyewe hawana umilisi wa lugha, na visaidizi vya Kiswahili katika kufundisha msamiati katika darasa la tatu huwa na utata mwingi sana. Goffin & Wilson (2001) wasemavyo kutengeza vinyago vya msamiati kama ndege na wanyama huwa na ugumu. Msamiati wa nyumbani huwa haufunzwi vyema. Uelewekaji wao huhitaji utumizi wa visaidizi halisi ili uboreke. Walimu mara nyingi hawatekelezi haya. Aidha, kwa sababu ya kukosa ubunifu wakutengeneza visaidizi hivi. Jambo hili linakera na kuchukiza kwani sote tunaohusika kwa kufunzwa na kujifunza lazima tutie bidii kujadili, kuelewa msamiati wote, kutatua matatizo ambayo yanatukumba baadaye. Nao Kahmi & Catts (2006) wanasema kuwa msamiati wa matunda, vyakula, ndege, wanyama, mavazi, mapambo na magonjwa hautofautishwi kwa sababu ya kukosa kutumia visaidizi vya kufundisha na kuhakikisha uelewekaji wa msamiati. Silibasi ya shule za msingi inahimiza ufundishaji wa msamiati au lugha kwa ujumla katika uzingatifu wa stadi zote za lugha

ambapo wakati mwingi stadi za kusikiliza na kuzungumza hazitiliwi maanani kama zilivyo stadi za kuandika na kusoma. Stadi za kusikiliza na kuzungumza huhitaji vifaa halisi ili kueleza msamiati vizuri; utumizi wa visaidizi kama inavyoeleza silibasi lazima itekelezwe ili ubunifu wa mwalimu uboreshe somo na uelewekaji wa msamiati.Hili ni jambo la lazima.

## 1.6 Umuhimu wa kushughulikia utafiti huu

Umuhimu wa utafiti huu unatokana na utumiaji wa visaidizi katika kufundisha somo la Kiswahili. Matumizi bora ya msamiati yaendelezwe kwani kufunza vyema awali ni bora kuliko kuyarekebisha makosa baadaye. Umuhimu wa utafiti huu ni kuthibitisha dhima ya visaidizi katika kuboresha uelewekaji msamiati katika shule za umma za Kaunti ya Kisumu Mashariki, Kenya. Somo la Kiswahili lifunzwe kwa motisha ili kubadili mielekeo hasi kuhusu somo hili. Silibasi ya Kiswahili ime orodhesha visaidizi ambavyo vinahitajika katika kila darasa. Hivyo ni vyema walimu kuzingatia hayo. Msamiati mwingine huwa na utata kama vile unaohusu wanyama wa porini, ndege wa porini, miti na matunda yake, mavazi na hasa katika darasa la tatu.Hivyo, walimu wanahijika kuzingatia mbinu mwafaka na visaidizi vya kufanikisha uelewekaji wa msamiati kwa urahisi.

## 1.7 Upeo na Mipaka Ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kaunti ya Kisumu mashariki na matokeo yake hayatawakilisha changamoto zote za shule za umma nchini Kenya.Matokeo ya utafiti huu yatachukuliwa kama vidokezo na sio kauli ya mwisho .Darasa la tatu ndilo ililoteuliwa katika utafiti huu na sio madarasa mengine.

## 1.8 Upungufu Wa Utafiti huu

(1) Utafiti huu utajikita katika matumizi ya visaidizi vya ufundishaji msamiati wa Kiswahili katika shule za msingi za umma Kisumu Mashariki. Huenda hamna ukuruba na wilaya nyingine.

(2) Utatifi huu utashughulikia shule za msingi katika shule za umma Kisumu Mashariki na huenda hauna uwiano na wilaya nyingine.

## 1.9 Kiunzi Cha Dhana

Kulingana na Bass na Contact(2005) ufundishaji unaotumia vifaa husaidia kuelekeza utambuzi wa talanta na kuwawezesha wanafunzi kupata uwezo wa ubunifu.Kulingana na Blooms(1956) kilele cha ujifunzaji dhana ni katika kupitia mtihani.Kupata majibu mwafaka kuhusu haya ni sharti ufundishaji na ujifunzaji utendeke.Orlich(2001) anatambua mwelekeo wa utendaji kazi wenye viwango viwili ambavyo ni muhimu vitekelezwe ili kupata matokeo bora.Kwanza kusaidia wanafunzi kuelewa na kufikiri.

### 1.9.1 Matokeo bora ya mtihani yatapatikana ikiwa :

1) Wanafunzi watapata motisha wanapofunzwa.

2) Visaidizi vitakuwepo ili wanafunzi waingiliana navyo.

3) Walimu wakizoea kutumia vifaa.

4) Umri na mazingira vitazingatiwa.

### 1.9.2 Hitimisho la Kiunzi cha dhana

Kiunzi hiki kinaonyesha matokeo bora husababishwa na mwingiliano wa walimu,wanafunzipamoja na vifaa husika.Mwingiliano huu wa vifaa na wanafunzi unahitaji maadili bora makini na umilisi somo ili matokeo bora yapatikane.Wenglisky(2002)anasema kwamba matokeo ya wanafunzi huhitaji mpango wenye ujuzi wa mahususi kufunza jinsi kiwango hicho kinavyohitajika  na utumizi wa visaidizi.

## 1.10 Nadharia Ya Utabia

Nadharia ya utabia ilielekeza utafiti huu. Nadharia ya utabia iliasisiwa na Harmer (1996).Katika utabia, utafiti huu ulifanywa katika mipaka ya ujenzi wa mielekeo katika nadharia ya utabia. Harmer (1996)ndiye aliyeiasisi huko Marekani. Inafaa msamiati ufunzwe vyema kuliko kukosoa makosa yaliofanyika awali. Kwani misingi bora awali huzuia utata wa kurekebisha makosa yaliyofanyika. Kutaja, kugusa, kutazama na kuona visaidizi halisia hubadilisha kule kubuni mambo ambayo huwezi kueleza vizuri. Utambuzi wa msamiati katika mazingira ili kujenga tabia sahihi ya lugha lengwa. Mwalimu atumie visaidizi ambavyo vinasaidia kuelewa msamiati bila kupotosha uelewekaji. Makosa ya kufunza awali yatakuwa na ugumu kuyarekebisha, baadaye atuzwe anapopata dhana kwa usahihi. Mwalimu ndiye anayeongoza na kuelekeza matukio darasani, naye mwanafunzi anayafuata maagizo. Visaidizi husaidia mwanafunzi kujifunza kwa urahisi na kuelewa dhana vizuri. Nadharia hii iliasisiwa mnano miaka ya 1920 (Harmer: 1996) kule Marekani. Hata hivyo, ilishamiri sana katika miaka ya 1950 hadi miaka ya 1960. Baadhi ya vipengele vya nadharia hii vingali vinatumika hadi sasa.Nadharia hii imejengwa katika misingi ya nadharia ya saikolojia utabia.Ufuasi wa nadharia hii ya utabia unaweza kudumu ikiwa utaigwa, kurudiwarudiwa na kutuzwa. Tabia isiyorudiwana isiyotunzwa hufifia. Kwa misingi hiyo ya nadharia ya utabia huwa:

- Mbinu zinazotumika kujenga tabia ya kawaida ya binadamu (kama vile kuendesha baiskeli) ndizo zinazotumika kujifundisha lugha ya pili.

- Jambo analojifundisha mtu kwanza, litayaathiri yale atakaloyofundisha baadaye.

- Mwanafunzi wa lugha apaswa kuyakariri matamshi mema (sanifu) ya miundo ya sentensi, mazungumzo, drili za aina mbalimbali ili kujenga tabia sahihi ya lugha lengwa.

- Mwalimu apaswa kutoa mifano mizuri ya kile anachotaka wakiige wanafunzi.Akikosea haitakuwa rahisi kusahihisha (tabia ya awali, na huathiri tabia ya baadaye) mwanafunzi arudie kipengele alichofunzwa na atuzwe kila akipatapo kwa usahihi.

- Makosa ni kikwazo cha kujifunza lugha ya pili (tabia nzuri). Makosa yapaswa kukatizwa na kuadhibiwa ili yasirudiwe tena. Makosa haya ni kama athari za lugha mama.

- Ufundishaji wa sarufi ya lugha ya pili huendeshwa kwa kukariri tungo zilizo na miundo ya kisarufi inayofundishwa. Wanafunzi wakizoea miundo inayohusika, itakuwa rahisi kung'amua kanuni zinazoitawala bila tatizo.

- Jukumu la mwalimu ni muhimu sana nalo ni kuongoza kila tukio darasani, jukumu la mwanafunzi ni kufuata maagizo. Nadharia ya utabia ni pana mno. Inawezekana kuwa hatujaeleza vipengele vyake vyote.

Mihimili hii ilisaidia katika kuthamini utumizi wa utumiaji, visaidizi kwani unachangia pakubwa mno katika uelewekaji wa dhana. Mwelekezi anapotumia visaidizi hivi katika kila somo na kuwa mtindo, basi uzoefu huyo huleta mvuto kwa wanafunzi. Dhana hazisahauliki hivo ikawa rahisi kukumbuka yaliyofundishwa. Mihimili hii ilisaidia katika kutunga hojaji, kukusanya data na kuchanganua data.

## 1.11 Mgofu Wa Utafiti

(i) Uchunguzi katika ufundishaji na ujifunzaji somo la Kiswahili katika shule za msingi hutegemea jinsi mwalimu anavyojiandaa na kutengeneza visaidizi vya ufundishaji ili dhana zieleweke.

(ii) Vigeu huru vya utafiti huu ni: mbinu ya ufafanuzi, mbinu ya utambuzi wa kitajiriba, visaidizi vya kufunzia na vitabu mwafaka.

(iii) Vigeu tegemezi vya utafiti huu ni matokeo bora ya mtihani, kazi maridhawa, kubadilisha mielekeo, kuboresha uelewa wa lugha na uzoefu wa kupenda kusoma vitabu vya Kiswahili.

Mchoro 1: **Kiunzi cha dhana**



## 1.12 Fasili Ya Istilahi

**Dhana:** Fikra iliyojengwa kwa mihimili fulani.

**Ensiklopidia:** Encyclopaedia

**Expository**: Fafanuzi /elezi, maelezo

**Heuristic**: Utambuzi wa kitajriba

**Kiunzi**: Mhimili mgofu

**Nyenzo:** visaidizi

**Mbinu:** Njia/Utaratibu

**Mfawidhi**: Mwalimu mjuzi wa kazi fulani

**Mwelekeo-fikira:** Mtazamo wa mtu kuhusu jambo fulani. Mwelekeo fikira unaweza kuwa chanya au hasi.

**Pendekezo:** Mawazo yanayotolewa na mtafiti kama msingi wa maswali au nadharia tete anayokusudia kufanyia utafiti. Pendekezo huwa kama ombi la kufanya utafiti.

**Teknoelimu**: Matumizi ya teknolojia katika maswala ya elimu.

**Uhalali:** Uthatmini

**Uaminifu**: Ukweli wa udhabiti

**Kutathmini** Kuhakikisha kwamba visaidizi vinatumika kufundisha

# SURA YA PILI: YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Elimu ni jambo la muhimu na haki ya binadamu wote (Washington: 2011). Elimu ni ufunguo wa kudumisha maendeleo ya nchi yoyote ile. Ndio ufunguo kwa uchumi. Serikali ya Kenya imeonyesha umuhimu huu. Katika mwaka wa 2003, serikali ilianzisha mfumo wa elimu ya bure katika shule za msingi ili kuhakikisha kila mwanafunzi hanyimwi haki yake ya elimu. Visaidizivya kujifunzia vimeundwa kuwakilisha hali halisi kuwawezesha walimu kufunzia wanafunzi kuelewa dhana zinazokusudiwa kueleweka.Kuwakilisha hali halisi kwa njia ya kutumia visaidizi au vyombo vya kufunzia na kuondoa utata, ili dhana hizo zieleweke kwa urahisi. Mwanafunzi hupata nafasi teule anapopata nafsi ya kuona na kubuni dhana inayozungumziwa kwa uhalisia. Visaidizi vya kufunzia vina umuhimu na ni vyombo ambavyo husaidia kuleta motisha katika kazi ya mwalimu na mazingira ya kujifunzia. (Kathleen: 2012).

## 2.1 Changamoto za kutumia visaidizi vya ufundishaji

Birgen (2005) anatambua kwamba mwanafunzi hupata mwingiliano wa visaidizi kwakutazama, kusikia na kuhusika katika somo darasani. Visaidizi hivyo vitatumika kufunzia somo na kurahisisha uelewekaji dhana kwa upesi. Ataweza kuchunguza uelewaji dhana wa wanafunzi kwa jinsi wanavyojibu maswali na kuuliza maswali. Walimu wajitayarishe wanapovitumia visaidizi kwani vinaweza kuleta utata na kuwa vizuizi vya somo kuliko kusaidia kueleza msamiati. Allinder (2001) anasema katika lugha,walimu watumie visaidizi hivyo vizuri ili wanafunzi wapate kuona au kuelewa jinsi mwalimu alivyopanga kufunza. Kulinganisha mambo walionayo mazingirani mwao na yale mapya wanayokusudiwa kufunzwa ni bora zaidi kuelekezwa hivyo. Mogeni (2005) alitambua kwamba kuna shida kupata hata vitabu vya kufunzia historia shule za upili huko Transmara. Naye hakujishugulisha na visaidizi vya aina nyingine yoyote. Anahimiza visaidizi husaidia kueleza dhana na ukosefu huzua utata tele. Riley (2005) alitambua kuwa vitabu ndivyo vinavyopatikana katika utafiti wake wa somo la Jeografia na visaidizi halisi havikutumika kwa njia inayofaa. Visaidizi hivyo alivyovitaja vikipatikana alisema walimu

ndio wenye ruhusa ya kuvitumia na wala si wanafunzi, katika Wilaya ya Kisii. Hivi ni kusema wanafunzi hawapati nafasi ya kuingiliana na visaidizi hivi basi kuzua utata wa kushika, kuona na kuguza. Utafiti huu utadhibitisha kuwa visaidizi ni muhimu katika kufunza dhana zozote. Orasanu (2001), anasema kwamba mashirika ya ujifunzaji yamekosa visaidizi vya kujifunzia. Anasema vitabu na ubao ndivyo hutumika sana. Visaidizi vingine havipatikani na havitumiki kufunzia somo. Anadhibitisha kuwa ubao sio kifaa pekee cha kufunzia. Visaidizi vingine pia husaidia kuelewa msamiati.

Njogu na Nganje (2006) katika utafiti wao wanaeleza jinsi walimu huchagua visaidizi vya kufunzia na ufundishaji wa kiswahili na pingamizi za utumiaji wa visaidizi vya kufundisha somo.Walitambua kuna ukosefu wa kuwa makini, karakana za utengezaji visaidizi hivyo, mielekeo hasi ya walimu kuhusu Kiswahili na sehemu za kuhifadhi visaidizi vichache vilivyotengenezwa au kununuliwa. Mogeni (2005) alitafiti kuhusu matumizi ya visaidizi vya kufundisha Kiswahili katika shule kadha za wilaya ya Transmara. Alitambua kwamba walimu wana ujuzi duni katika matumizi ya visaidizi katika somo la kiswahili, uhaba wa visaidizi vya kutosha vyenye maana na vya kutosha kutumia kufundishia kiswahili, ubunifu wa kutengeneza visaidizi umeadhihirika mno, kukamilisha silabasi kumeleta utata, wakati wa kutengeneza na kutumia visaidizi hivyo jinsi inavyotakikana.Utumiaji mbaya wa visaidizi huleta kutoeleweka kwa dhana. Utafiti huu utathmini jinsi visaidizi vinavyosaidia uelewekaji dhana. Kulingana na tafiti za awali ni wazi kuwa visaidizi vya kufunza msamiati havitumiki jinsi vilivyoorodheshwa katika silibasi, chaki, ubao na vitabu vichache ndivyo vinavyotumiwa kwa uchache tu. Warsha za kutengeneza na kutumia visaidizi hivyo hamna, sehemu za kuhifadhi visaidizi vilivyomo hamna, idadi ya wanafunzi na mtihani wa kitaifa huchangia pakubwa kutotumia visaidizi hivi. Utafiti huu utatathamini jinsi utumiaji visaidizi ni muhimu katika kufunza msamiati wa Kiswahili na jinsi dhana huweza kuelewa kwa urahisi. Mielekeo hasi kuhusu somo hili itapunguka na matokeo bora yatapatikana. Vile vile matumizi ya msamiati katika maingiliano yataboreka.

Njogu na Nganje (2006) walitafiti kuhusu mielekeo na uelewa wa walimu na wanafunzi kuhusu vipindi vya redio na kudadisi pia sababu za mielekeo hiyo. Utafiti huu utachunguza mielekeo na uelewa wa walimu na wanafunzi kuhusu matumizi ya visaidizi katika

msamiati wa somo la kiswahili kwa jumla. Republic of Kenya (2006a) inasema kwamba mashirika yameundwa na binadamu (wafanyikazi na vitu vingine ambavyo si wafanyikazi (rasilimali). Uelewa wa dhana katika ujifunzaji unanahitaji visaidizi halisi ili msamiati ieleweke vizuri, nayoshabaha ya somo itafikiwa. Hivi ni kusema kwamba ni wazi kwamba, visaidizi vya kufundishia huchangia pakubwa katika kurahisisha uelewekaji wa msamiati katika shule kama njia moja ya kufanya shule kufaulu. Visaidizi hivi ni vitu vya muhimu sana ambavyo huleta matokeo bora kwa wanafunzi wote.

## 2.2 Sera za ukanguzi matumizi ya visaidizi vya ufundishaji

Kenya National Examinations Council (2005) inalalama kuhusu matokeo duni ya mtihani huu wa kitaifa (KCPE). Imetaja jinsi mahitaji ya silibasi hukumbanana na changamoto nyingi. Walimu huandaa somo bila visaidizi muhimu vya ufunzaji na basi msamiati hueleweka kwa njia finyu mno. Baada ya walimu kuteua masomo katika silibasi zao huwa hawajitayarishi vyema. Kwa mfano: kutengeneza maandalizi ya somo na kuteua visaidizi mwafaka vya somo. Hivyo changamoto huwa nyingi ndiposa utafiti huu umejikita kutafiti kuhusu utumiaji visaidizi vya kufundisha msamiati katika somo hili. Somo hili linahitaji kufunzwa kwa kuzua hisia, misisimuko wa kuwahusisha wanafunzi wote. Krashen (2003), anasema kwamba lugha ya Kiswahili ikifunzwa kwa kuwahusisha wanafunzi, basi wataibuka kuwa watenda kazi wenyewe na wabunifu. Visaidizi halisi huzua uchangamfu wa kujifunza lugha, huzua motisha na uelewekaji bora wadhana kama msamiati. Kulingana na Birgen (2005) visaidizi halisi huguswa, hushikwa ili msamiati ukumbukwe kwa urahisi kuliko kile kilichobuniwa ama kuzungumziwa tu.

PDSI (Plan, Do, See, Improve) ni njia ya kufunza ambayo imejikita katika utafiti wa Penny (2000) ambao umesisitiza haja ya wanafunzi kufanya mipango bora ya ufundishaji na mazoezi ambayo yanahusu kujionea wenzao na kuboresha mazoezi hata zaidi kwa ujifundishaji halisia kwa kutenda. Ni jambo la muhimu kujua kwamba hamna mwanafunzi ambaye ni mjinga na asiyeweza kujifunza, wengine huwa wanachukua muda (Republic of Kenya: 2006b), PDSI sharti itimiziwe kabisa ili ihakikishe kwamba wanafunzi wote wanaweza kupata au kuelewa dhana zote walizofunzwa.

Kama mikakati ya kutimiza PDSI, kufunza lugha kwa mawasiliano (CLT) ulibuniwa.Jambo la muhimu ni kuboresha utendaji kazi wa wanafunzi kwa kuendeleza umilisi wa miingiliano ya watu vile vile umilisi somo.Changamoto za ufundishaji kwa njia za kitamaduni (Becher: 2005) Kulingana na umilisi wa lugha ushupavu ni ujuzi wa mzungumuzaji na jinsi anavyoweza kujieleza katika sherehe tofauti; kwa maneno mengine ni uwezo wa kuzungumza kwa usawa kijumla katika miingiliano ya utamaduni katika muktadha wa mawasiliano. CLT inaamini kwamba kuwapa wanafunzi nafsi ya hali halisia ya utumiaji wa visaidizi vya ufundishaji darasani ni njia moja nzuri ya kujiendeleza. Hata hivyo si kusema kwamba wanafunzi wahimizwe katika uzungumzaji na kijiendeleza na kusahau kutilia mkazo katika sarufi iundao lile ambalo wanazungumzia.

CLT haikubaliani na wazo la kufunza lugha kwa kueleza dhana na drili za sentensi kwani huku kutazua hali ya kuwa na uwezo wa (umilisi lugha) na hawawezi kujielezea katika hali halisi katika maingiliano ya kila siku. Haya ni kweli kwani mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili sharti ajue jinsi ya kuitumia lugha katika mawasiliano halisi. PDSI inawezakufikiwa ikiwa upangaji, ufanyaji kazi, utazamaji, na urekebishaji utafanywa. Hivi ni kusema utendaji kazi utadhibitika na sio tu kuzungumza. (Wells: 2006) utendaji kazi huzua ubunifu, ari ya kufanya mazoezi mwafaka na kuwezesha wanafunzi kutumia lugha sahihi. Katika mpangilio wa Willis Model” wa utendaji kazi kama anavyorejelea (Wringe: 2010) kiunzi hiki kimegawanywa katika hatua tatu.

Katika hatua ya kwanza, mwalimu anaeleza mada na anaweza kuwasaidia wanafunzi kukumbuka somo la awali litakalowasaidia katika utendaji kazi huu. Hii ni kama vile kutazama kanda za video za watu wakitenda kazi inayohusika ya kuonyesha ujumbe au visaidizi vingine. Hii huwawezesha wanafunzi kubuni wanalotarajia, wanafunzi wanaweza kuchukua daftari na kuandika kazi fulani na kuandika daftari kazi fulani au kutumia mada kujitayarisha kwa kazi. Hatua ya pili ni kupanga kazi katika makundi au wawili wawili. Baada ya kujadili hoja, wao hutoa ripoti ya kundi husika. Mwalimu huwa mwelekezi, msaidizi kisha wana kikundi huwasilisha kazi yao kwa mbinu ya kueleza au kusoma waliochoandika. Wanafunzi wengi husikiza na kukagua kazi ya makundi hayo.

## 2.3 Udhaifu na ufaafu wa matumizi ya visaidizi vya ufundihsaji

Mwalimu na wanafunzi wengine hujadili na kutoa maoni yao. Hatua ya mwisho ni ile ya ukaguzi. Visaidizi vya kufunzia vimefanywa katika makundi mbalimbali. Kundi la visaidizi vilivyochapishwa, visaidizi halisi, visaidizi vya kutazama na mwisho visaidizi vya kusikiliza. Marine na Hilles (2008)wanatambua kuwa visaidizi hivi ni vile vinavyoweza kuonekana na wanafunzi ambao huwasilisha ujumbe fulani kwa madhumuni ya kufunzia darasani. Aina hii ni kama picha, kadi za umeme, michoro, ramani, chati, visaidizi halisi. Ni dhahiri kwamba matumizi ya visadizi huchangia katika ufanisi wa kufundisha msamiati ya Kiswahili. Kyriacou (2001)anatoa kauli kwamba ni vyema kutumia vinango na kuvielewa kadri unavyovirejelea. Mwalimu anaweza kueleza msamiati fulani kwa urahisi atumiapo visaidizi na uelewekaji wa msamiati ukafaulu. Visaidizi halisi huibua motisha na husaidia katika uelewekaji wa msamiati kwa urahisi mno. Wanafunzi hushika na huona na kuweza kurudiarudia utendaji huo, hapo basi uelewekaji ukawa rahisi na kuweza kukumbukwa vyema. Visaidizi halisi vikilinganishwa na neno husika huwa rahisi kueleweka kuliko kubuni jambo katika ubongo (Just na Carpenter: 2002). Mwalimu huzungumza kwa uchache na mwanafunzi ndiye mtenda kazi. Utendaji kazi unahimizwa katika mfumo mpya wa elimu. Wanafunzi wawe wavumbuzi wanapoingiliana na visaidizi katika somo.

Grove na Hauptfleisch (2008) wanapendekezakuwa picha kwa mfano ni “muhimu na lazima zitumike katika ufundishaji wa vipenge vya lugha”. Mwalimu anaweza kutumia picha katika mawanda yote ya kufunza somo la msamiati. (Kwa mfano: katika utendaji kazi, kutoa maoni, kuwasilisha kazi, kufanya marudio). Ikiwa mwalimu ataweza kutumia picha kwa hali ya uchangamfu na ucheshi, wanafunzi watachangamkia somo na kuhudhuria kwa njia ambayo kusomesha kwa utamaduni kwa utumiaji vitabu, ubao, uandikaji wa sentensi ubao haungewezekana (Nunan: 2009). Kanda za video zinaelezwa kuwa “models and devices” ambazo hunaswa na hueleza picha inavyonuiwa kuelezwa. Mwalimu huweza kubadili njia na mtindo wa kufunza na kubadili mazingira ya darasani kwa upesi kama ilivyotarajiwa. Kwa upande mwingine huibua hisia za mwanafunzi humzuzua kimawazo, hupunguza uchovu, humpa motisha ambao humfanya kujitumbukiza

katika ujifunzaji, hivyo kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza. Baadaye inakuza vipawa vyakujieleza na kuzungumza hadharani. Visaidizi hivi husaidia uelewekaji wa msamiati na sauti zenye mteremko na mshuko wa sauti uliotolewa katika kanda.

Kama ilivyorejelewa na kamusi ya oxford ya wanafunzi, nyimbo hueleza msamiati kwa vipande vidogovidogo vya muziki vyenye maana inayokusudiwa kueleza msamiati fulani. Kulingana na Gelzheizer na Meyers (2008) marejeleo ni muhimu kwa uwakilishaji wowote ule wa lugha/grama iliyo na maana kamilifu katika utendaji kazi, katika nyimbo hasa utamu unaowasilisha hekima ya kitamaduni, nazo nyimbo ndizo hasa moja ya jambo la busara na la kutamaduni lililo bora zaidi katika asilimia za marejeleo. Chall, Jacobs na Baldwin (2007) walipendekeza kwamba nyimbo zinaweza kufanyiwa uwasilishaji marejeleo, na kutiliwa mkazo kama vyombo au njia ya kufunzia stadi zote za lugha, na kama chombo cha kuwakilisha vitu muhimu vya dhima, utamaduni ambao umepita au shida usasa.

Visaidizi vya kusikiliza (Audio Visual Aids-Video) vya kufundishia vinaweza kueleweka kama "vyombo vinavyotazamwa macho na kutoa sauti ilikuwasilisha ujumbe." Kwa hivyo kuvitumia ni muhimu sana kwasababu husaidia kuhifadhi hali ya juu na motisha katika somo, kupata wanafunzi kutumia lugha, huboresha kuhudhuria kwa wanafunzi na utumizi katika daraja zote za ujifundishaji. Fikira hizi zimeungwa mkono na kusaidiwa na Marine & Hilles (2008). Fikira kwamba "Video inauwezo wa kukuza usomaji lugha na kufanya iwe ya kusisimua na mwafaka au ifaavyo." Kama ilivyojadiliwa Pretorius (2002) anasema kwa wanafunzi wa umri wa miaka mitatu hadi minane, video ni njia mwafaka ya kusoma, mihimili ya lugha. Wanafunzi wachanga wangali wanajifunza kuhusu ulimwengu uliowazunguka. Vilevile wanafunzi wachanga hufurahia masimulizi ya hadithi, kuona video tena na tena, ambapo wao hupata ushupavu katika kurudiarudia na kuona video mara nyingi. Kwa wanafunzi wachanga kutazama video kuna faida nyingi sana kwani "video huwasiliana kikamilifu zaidi ya njia nyingine yeyote" Tomlinson(2012). Wang (2009) aunga wazo hili na kudokeza kuwa video huwasilisha marejeleo kwa njia ambazo redio haiwezi. Wanafunzi waweza kuona mzungumzaji, mahali alipo na kazi ambazo anafanya."

Watafiti wanakubaliana kuwa kule kuvutia ubongo kupokea elimu huwezekana asilimia themanini na tano kwa hisia za kuona na kusikiza.Elimu hupatikana katika madaraja matatu. Moja kwa moja, visaidizi au vifaa vya kufunzia ni muhimu sana kuendeleza somo. Visaidizi hivi husaidia kupokeza ujumbe, uelewa wa somo na ulinganifu wa maana. Dhana mpya ya elimu inadai kwamba visaidizi hivi vinawawezesha wanafunzi kutumia nyenzo zote ambazo huhusisha stadi zote ili kuwawezesha kuwa wabunifu, kupata hali halisi ya mambo, kutambua maana yenyewe na kuzidisha uvumbuzi mambo. Utafiti huu utajaribu kutambua umuhimu wa kupokea dhana mpya na mabadiliko. Mojawapo ya maswali ya utafiti ni kudhihirisha kwamba visaidizi vya ufundishaji husaidia kuelewa maana au kwamba uelewekaji wa somo hukuzwa kwa kutumia visaidizi au vifaa hivi.

Sigmund (1920) aliibua dhana ya mchezo kwa kung'amua kwamba mchezo ni tiba katika kitabu chake cha 'Beyond the Pleasure Principle'. Katika kazi hii Freud anaelezea kuwa mchezo wa watoto ni njia moja ya kurudia na kukariri matukio ya awali ambayo yalimkera. Katika mchezo wake, mtoto huweza kuyabadilisha matukio hayo na akayarekebisha kwa njia iliyo burudani kwake. Maria Montessori Mtaliano aliyekuwa mtaalamu wa sera ya elimu mapema miaka ya 1900 alisema kwamba: michezo ni kazi ya watoto" kulingana na njia ya Montessori ambayo hadi sasa hutumika katika shule za kibinafsi, watoto huiga na kubuni. Montessori anakiri kwamba kucheza kunaibua hisi za utumizi wa mikono katika kugusa visaidizi vyote ili kujifunza kuelewa na kukumbuka. Watoto hujifunza katika viwango mbalimbali, mwalimu naye huwa mwelekezi ili mtoto acheze huku akijifunza. Dewey (2009) anajulikana kama mwanzilishi wa viwango maalumu vya ukuaji wa watoto.Viwango hivi vinadhibitisha wazi jinsi mchezo unahusiana navyo. Ukuaji wa akili huibuka watoto wanapopitia viwango hivi vya mwingiliano au uwezo wa kuingiliana na mazingira waliyomo ili kuweza kuridhika na haja ya kibinafsi, mchezo wa kuigiza au kubadilisha hisi za kibinafsi kuweza kuridhika na hoja za mazingira au kazi.

Lev Vygoskyalitoa maoni kwamba michezo ndiyo njia inayotumiwa na watoto kukua kisoshiolojia. Katika mchezo, watoto huweza kuingiliana na kujifunza kwa kutumia lugha na uakifishaji michezo ya kuigiza. Vygostsy alijulikana kwa ubunifu wa ZPD au (zone of

promiximal development) watoto wanapohitaji wenzao kucheza au rika lao vivyo hivyo wanahitaji mwingiliano wa watu wazima wanapoingia na kukariri kila mbinu ya kisoshiolojia na huwa tayari kufunzwa mambo mapya ili wakue. Vivas (2011) anasema kuwa mistari huridhisha macho lakini ishara na picha huboresha akili, tunawazia kuhusu picha na ishara katika akili zetu kwa kutumia maneno, hivyo basi maneno picha na ishara zikiwa pamoja ni njia bora zaidi ya kuwasilisha mawazo. Washington (2011) anaendelea kusema kuwa maandishi yakichapishwa chini ya picha, maelezo hayo huonyesha umuhimu wa maarifa ya kawaida yanayowasilishwa katika picha. Maandishi yakiwa ubavuni mwa picha huonyesha sifa na umuhimu wa bidhaa au huduma inayorejewa katika picha. Gazeti la Nation (13 Jan 2011) lilinukuu waziri wa elimu Kenya akisema kuwa licha ya kuwa kiswahili ni lugha ya taifa, matokeo ya somo hili katika mtihani wa kitaifa (KCPE) huwa mabaya mwaka baada ya mwaka. Sababu zilizotolewa katika gazeti lenyewe ni kwamba mbinu za ufundisaji zinazotumiwa na walimu wengi wa kiswahili ni duni, na hivyo huleta matokeo duni. Walimu huingia darasani bila visaidizi au vifaa hivi vya kufunzia.Uelewekaji wa msamiati katika utumiaji vifaa, mwelekezi anahitaji kuvitumia na kujitayarisha kabla ya kwenda darasani. Mwelekezi aweze kutumia mwamko mapya wa kufunza ambapo mwanafunzi anapata nafsi ya kuingiliana na vifaa na mwalimu kuwa mwelekezi.

Nunan (2009) anatambua kuwa asimilia kubwa ya ujumbe ambao tunawasilisha hupitishwa kwa kutumia hisi ya kuona na inayosalia ni kupitia hisi ya kusikia. Kuona ndiko kuamini na kuhakiki mambo. Penny (2000) anafafanua kwamba kutumia hisi ya kuona katika mawasiliano ni jambo muhimu sana kwa vile inasemekana kuwa watu huhifadhi asilimia ishirini ya wanachokisikia na asimilia hamsini ya mawasiliano yanapohusisha hisi ya kuona na kusikiliza. Visaidizi vya kufundisha ni muhimu na vinasaidia katika kufasiri ujumbe na uifadhi katika ubongo zaidi ya kusikiliza. Jambo la kutotumia visaidizi miongoni mwa walimu huzuia kueleweka kwa msamiati. Utafiti wetu utachunguza sababu za kudidimia huku kama njia moja ya kufanya wanafunzi kuelewa somo na kulihifadhi katika bongo zao. Utafiti huu utajikita katika kutathmini sababu za kutotumika kwa visaidizi hivyo katika kila somo na walimu wahusika. Nunan (2009) asema kuwa walimu wengi wamejishugulisha na upitaji wa mtihani drilli zinaendelea bila

kufunza mwanafunzi awe wakujiendeleza,kufahamu mambo na kujimudu vile vile katika somo la Kiswahili.

Kwa mfano: shule zilinafanya vizuri katika mtihani wa kitaifa ilhali wanafunzi hawafahamu mambo na hawapati nafasi ya kuchambua mambo kwa kiina,kulinganisha, kujieleza au kutambua mambo kadhaa. Basi lengo kuu wakati huu ni kuupita mtihani bila kupata ufasaha wa kutumia lugha vyema na kujikimu inavyotakikana katika maendelezo ya lugha taifa. Waliofunzwa lugha vizuri wanaimudu vyema, kujiendeleza na tunapata wanafunzi wanao uwezo wakuwa, wahutubi, wandishi na wasomaji habari. Utata huu wa kutowafunza msamiati katika somo la kiswahili kwa ustadi na visaidizi vifaavyo unaibua upungufu wa wandishi na wahutubi.

Su na Hong (2007) wanaeleza bayana kuwa lugha ya picha hukamilishana kimaelezo, kiujumbe na kimuktadha.Visaidizi zaidi vya kufundishia kama vile vitabu vya ziada, vitabu vya kawaida, walimu au visaidizi vingine ambavyo vinahitajika au kuongezwa katika viwango vyote vya elimu na vyuo vikuu. Wang (2009) nashauri kuwa ili ufundishaji na ujifundishaji wa msamiati wa Kiswahili ufaulu inavyotakikana sio tu kupita mitihani lakini kuelimika kabisa na kupata umilisi wa lugha jinsi inavyotakikana.

Wringe (2010),ananukulu kwamba ,“Watoto wanahitaji kufunzwa, kujua na kuwa na uwezo”. Haifai wao kufanyiwa ufundi katika ukuaji. Kama alivyosema Quist (2005), “Mwanafunzi si mtu anayechagua sehemu katika mazingira. Ujifunzaji unaweza kuibuka mahali mwanafunzi anapohisi hitaji. Kujifunza ni kazi ngumu”. Kyriacou (2001) anasema, “Nimetambua kwamba kujifunza ambako kunasaidia katika kujenga tabia ni kule ambako wewe mwenyewe unavumbua na unajitolea.”Grove and Hauptfleisch (2008) anaweka wazi, “Kujifunza kwa ukweli, katika uhakika wa mwisho ni elimu inayotegemea uelewekaji wa kibinafsi.”

Chall, Jacobs,na Baldwin (2007) waamba kwamba kufunzwa kwa mpangilio dhabiti wa maeneo ya kujifunzia huleta ugumu kwa wanafunzi kuweza kuelewa au kuleta maana kwa mambo ambayo yamepangwa tu. Mwelekezi sharti apange mpangilio wa mafunzo ya masomo ili afikie wanafunzi wake na kuwezesha uewekaji wa dhana ili kufikia shabaha

kwa mielekeo itakayofanikisha uhuru wa kujadiliana, kubuni, mwingiliano na kuvumbua ukweli dhabiti wenyewe. Allinder (2001) ana msimamo kwamba walimu lazima wawe na ujuzi maalumu kuhusu wanafunzi katika mambo na kazi fulani na jinsi ya kupokeza na kufunza dhana hizo. Chall, Jacobs,na Baldwin (2007) wanasema kwamba kufunza ni tendo la kuwasilishwa kwa hali ya jambo halisia au lisilo halisia. Kwa hivyo tunapofunza ni lazima au ni vyema kujua wanafunzi na somo linalohusika. Ni vyema vilevile kujua jinsi ya kufunza kwa ujumla na hasa katika hali halisi na vipaji halisi vipasavyo katika hali hiyo au kwa dhana hiyo. Kule kubadilika kwa majukumu fulani kunamaanisha kwamba mwelekezi lazima aonyeshe ustadi wa vipaji fulani kuliko mwalimu. Foorman na Torgesen: (2001) nao wanasemamwalimu hunena, huelekeza, huuliza, mwalimu huzungumza kutoka mbele, mwelekezi  huelekeza na kutoa mwelekeo na kuibua mazingira mwafaka kumwezesha mwanafunzi kubuni maoni yake mwenyewe, mwalimu huzungumza lakini mwelekezi huzua majadiliano na wanafunzi Chall, Jacobs & Baldwin(2007). Mwelekezi lazima awe na uwezo wa kujadili na kupokea ujifunzaji mpya kwa kufululiza mawazo mapya hadi ambapo wanafunzi wanabuni jambo jipya au kutoa maoni yao.

Mazingira ya ujifunzaji lazima yawe ya kusaidia na kutoa changamoto za kufanya wanafunzi kutumia bongo vizuri Gelzheizer & Meyers (2008). Kule kuwatetea wanafunzi kuwa wenyeji wa shida na usuluhishaji kazi, si kwamba kila zoezi au suluhisho limetosheleka. Jambo la kutafakari mambo kwa kina linahitaji kutoweka kazi mbili kwa pamoja, ile ya kocha na mwelekezi ili kufanikisha hayo yote. Wananadharia ya Vygostkiwanasisitiza kwamba watoto wanahitaji kufanya kazi au zoezi ambalo watafaulu kwa usaidizi unaotolewa. Wanasisitiza kwamba, mtoto anahitaji, ambalo lazima litambuliwe na kukuzwa iwapo matumizi ya visaidizi yatatiliwa maanani. Hali na zoezi ni muhimu na lazima katika ujifunzaji wote kwa hivyo wanafunzi lazima wafanye zoezi halisi kila siku kwa sababu ya kuzua maana na hitaji Kahmi & Catts (2006).Katika kuleta maana, ieleweke mwelekezi ambaye ni mwalimu atafanya wanafunzi kufanya kazi pamoja kwa madhumuni ya kujifunza pamoja kama jinsi wanafunzi walio na vipaji au vipawa tofauti na tamaduni tofauti na wanahitaji kufanya mazoezi na majadiliano ili kuweza kusaidia kuelewa mambo au ukweli katika taaluma maalumu Krashen(2003). Hayo yote

yatafanyika mwalimu anapotayarisha visaidizi vya kujifunza na kutengeneza mazingira mwafaka ili kazi hii iwezekane na hapo wanafunzi wenye tofauti hizo watajifunza kwa urahisi kushika, kutazama na kukumbuka dhana zilizofunzwa kwa urahisi.

## 2.4 Muktasari wa yalioandikwa kuhusu mada

Yaliyoandikwa kuhusu vifaa vya ufundishaji kwa ujumla yametafitiwa kwa wingi nchini Kenya na nje.Mtafiti alilenga kutathmini matumizi ya vifaa vya kufundisha msamiati wa Kiswahili katika shule za msingi za umma, kaunti ya Kisumu Mashariki,Kenya.Mogeni(2005), Allinder(2001),Kathlen(2012),Krashen(2003)wasemavyo ufaafu uliopo wakutumia vifaa katika somo.Yaliandikwa kuhusu mada yalitambua kwamba kuna aina mbalimbali ya vifaa vya kufunza ambavyo vinachangia pakubwa katika uelewekaji wa dhana.Kuwepo kwa vifaa hivi hakudhihirishi kwamba kumefanya uelewa dhana kuwa kwepesi,lakini kule kutambua vifaa vinavyotakikana,wakati wa matumizina utumiaji wa vifaa kueleza dhana ndio muhimu.Vifaa vyote havipatikani darasani,lakini katika mazingira huwepo vifaa ambavyo huleta mwingiliano halisia na huboresha uelewa wa dhana vizuri.Patel & Mukwa, (1993),Mwangi,(1985) na wengine wanatambua kwamba utumiaji vifaa una changamoto zao kama vile fedha za ununuzi,utambuzi wa vifaa na njia mwafaka za kutumia visaidizi hivyo.Kathlen na wengine (2012) wanatambua kwamba utumizi wa vifaa hivi unaboresha matokeo ya mtihani.Hivyo kuzua pengo la kuziba kwani tofauti na kazi yangu in upeo, walengwa,njia za uchanganuzi na ukusanyaji wa data,mapendekezo.Utafiti huu unanuia kutathmini matumizi ya vifaa vya kufundisha msamiati wa Kiswahii katika kaunti ya Kisumu Mashariki,Kenya.

# SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI

Sura hii inajihusisha na uchanganuzi wa data pamoja na kujaribu kueleza sababu zinazozuia walimu kutumia visaidizi vya kujifunza na kufundisha msamiati ili kuboresha uielewekaji wa dhana inavyohitajika.

## 3.1 Mbinu Za Utafiti

Mtafiti alitumia utafiti wa kiidadi na kutathmini mbinu ya maelekezo kumwezesha mtafiti kuteua walengwa.Mbinu ya maelezo na kiidadi ilimsaidia mtafiti kupata ujumbe kuhusu utumiaji wa vifaa katika kufundisha msamiati wa Kiswahili pamoja na wanafunzi wa darasa la tatu.Best & Kahn,(1992).Utafiti ulihusu shule za msingi za umma zilizoteuliwa kwa bahati nasibu kutoka shule zote za kaunti ya Kisumu mashariki.Utafiti awali ulifanya kudhibiti vifaa vya utafiti. Ukusanyaji data,uchanganuzi,hitimisho na mapendekezo umeorodheshwa katika mchoro wa pili.

**Mchoro 2 : Muundo wa utafiti**



### 3.1.1 Hitimisho la kiunzi cha dhana

Vigeu tegemezi ni matokeo ya mtihani. Vigeu huru ni vifaa vya kufundishia msamiati. Vilevile vigeu viingilizi ni :

- Kiwango cha elimu,ueledi wa mbinu za ufundishaji
- Mazingira,umri na afya ni vigeu ingilizi.

Mwingiliano wa vigeu huru na tegemezi viliadhiriawa na vigeu ingilizi kama inavyo onyeshwa katika kiunzi dhana.Mbinu kusudi iliteua mwalimu mmoja wa darasa la tatu wenye tajriba.Uteuzi wa nasibu ndio ulitumika kuwa tena wanafunzi wa darasa la tatu ambapo mbinu hii iliweza kuchagua wanafunzi wa kila sampuli.

## 3.2 Eneo laUtafiti

Utafiti huu ulilenga kaunti ya Kisumu Mashariki na matokeo hayakuwakilisha shule za msingi zote za umma nchini Kenya.Wanafunzi wa darasa la tatu ndio waliohusishwa katika utafiti huu.Hojaji na mahojiano yalihusu walimu, wanafunzi, wasimamizi wa shule na wahusika wote katika jopo la elimu nchini Kenya ili kukabiliana na shida au utata wa kutoelewa msamiati fulani. Sababu za kutotumia video, vinyago na chati wakati wa kufundisha na ufundishaji kama inavyotakikana. Mtafiti alitoa mawazo hasa kwa washikadau wa elimu na wazazi kupata matokeo mazuri ya Kiswahili kutoka kwa wanafunzi baada ya kutathmini ufundishajiwa msamiati wa Kiswahili kwa matumizi ya visaidizi hivyo. Vile vile msamiati utumike vyema katika maingiliano ya watu katika jamii zetu.

## 3.3 Walengwa

Walengwa wa utafiti walikuwa shule za msingi za kaunti ya Kisumu Mashariki ,ambao walikuwa wanafunzi themanini na mbili,walimu wa Kiswahili kumi na watatu,darasa la tatu,walimu wakuu kumi.

Kwa vile si rahisi kufanya utafiti katika shule zote za umma katika kaunti ya Kisumu mashariki, ni shule kumi tu zilizowakilisha shule zote za msingi katika Kaunti ya Kisumu. Matokea haya yalitumika tu kwa baadhi ya shule za umma. Shule za kibinafsi

hazikuhusishwa kwa sababu  hadhi na jinsi utawala unavyofanyika ni tofauti na shule za umma. Nyingi za shule hizo hazina utaratibu wenye kanuni maalumu, kwani nyingi tu nia yazo ni kutengeneza pesa.

## 3.4 Uteuzi Wa Sampuli

Katika utafiti wa kiidadi na maelezo,Mugenda na Mugenda (2003);Cohen,Manion na Morison (2007) wanaeleza ni vyema kuchukua asilimia 10% hadi asilimia 20.0% ya walengwa wote kwa sampuli ndogo au kubwa.Ikiwa sampuli ina aina aina tofauti,sampuli ya kihasibu itafaa.Lakini sampuli kubwa hutoa aina mbalimbali za yaliotarajiwa katika utafiti.

**Jedwali 2: Idadi Ya Wanafunzi wa Kiswahili**

| Shule/Kiwango | Darasa la 3 |
|---|---|
| A | 75 |
| B | 80 |
| C | 85 |
| D | 90 |
| E | 80 |
| F | 75 |
| G | 80 |
| H | 85 |
| I | 85 |
| J | 90 |
| **JUMLA** | **825** |
| **10%** | **82** |
| Kila Shule | 8 |

Kiini: Kazi Ya Mtafiti (2013)

Idadi ya walengwa ilikuwa walimu thelathini katika shule za msingi za umma kama walivyoteuliwa katika maelezo haya.

**Jedwali 3:Idadi Ya Walimu Wa Kiswahili**

| SHULE/KIWANGO | WALENGWA | JUMLA |
|---|---|---|
| A | 3 | 1 |
| B | 2 | 2 |
| C | 3 | 1 |
| D | 4 | 1 |
| E | 3 | 1 |
| F | 2 | 2 |
| G | 3 | 1 |
| H | 4 | 2 |
| I | 3 | 1 |
| J | 3 | 1 |
| **JUMLA** | **30** | **13** |

Kiini: Kazi Ya Mtafiti (2013)

## 3.5 Visaidizi Vya Utafiti

Mtafiti alitumia vifaa vitatu katika utafiti huu. Hojaji, mahojiano na nakala za uchunguzaji somo. Matumizi ya visaidizi vilevile yalichunguzwa kudhibiti ubora (Creswell: 2003).

### 3.5.1 Hojaji

Hojaji ni vifaa vikuu vilivyo kukusanya data katika kazi hii. Hojaji tatu, za walimu wa Kiswahili, ya wanafunzi na ya walimu wakuu zilitumika. Hojaji zilikuwa na maswali funge na maswali wazi. Maswali wazi yaliwawezesha kujaza maswali halisi na maswali wazi yaliwawezesha walengwa kutoa maoni yao bila wasiwasi, na kujieleza kwauwazi.

### 3.5.2 Nakala ya uchunguzi

Nakala ya uchunguzi somo iliundwa ili ionyeshe jinsi hasa vifaa vinavyohitajika katika ufundishaji.Nakala ya uchunguzi ilisaidia mtafiti kupata data ya kuwepo kwa vifaa,na utumiaji wazo na hali halisia ya utumizi wa vifaa katika somo.Ujumbe uliododolewa kutoka kwa nakala ya uchunguzi ilitumika kueleza jinsi ilivyo darasani kuhusu utumizi wa vifaa kwa walimu na wanafunzi. Mtafiti alitumia nakala hii kukagua somo .

Nakala ya uchunguzi ilitumiwa kudadisi somo ili kuhakiki kama visaidizi hivi vilivyoorodheshwa vimetumika na kwa njia ipi.

## 3.6 Idadi ya walengwa

Wanafunzi walioteuliwa walikuwa wanane kutoka kila shule. Walimu wa Kiswahili walikuwa mmoja mmoja, ingawa shule 'B' ilikuwa na madarasa matatu. Idadi ya utafiti ni watu, vifaa au mtu binafsi anaye vipengee ambavyo mtafiti ana kusudi kutafiti. Mtafiti alijumuisha matokeo ya kazi hii. Gall et al, (2007). Mugenda na Mugenda (2003) Kisumu Kaunti ya Mashariki ina shule 825, walimu 30, walimu wakuu 30.

**Jedwali 4: Walengwa wa utafiti**

| Viwango | Idadi |
|---|---|
| Walimu wakuu | 30 |
| Walimu wa darasa la tatu | 30 |
| Wanafunzi | 825 |
| **JUMLA** | **885** |

Kiini: Kazi Ya Mtafiti (2013)

### 3.6.1 Utafiti wa awali

Mtafiti alifanya utafiti awali kabla ya utafiti halisi.Umuhimu wa utafiti awali ni kudhibiti vifaa vya utafiti ili kuhakikisha utathmini na udhabiti wa vifaa kwa kutambua kasoro na kuzirekebisha kabla ya utafiti wenyewe.Maswali yaliyoleta utata yalirekebishwa na kuundwa tena ili walengwa waweze kuyajibu bila utata.Utafiti ulifanyika katika shule moja ya umma na kuhushisha mwalimu mmoja wa darasa na mwalimu mkuu mmoja.Shule hii haikuwa moja ya shule lengwa.Darasa la tatu ndilo lililolengwa na siyo madarasa mengine.Wanafunzi walikuwa wanane kwa kila darasa.Mtafiti alitumia matokeo ya utafiti awali kuboresha vifaa hivyo vya utafiti.

Jedwali 4: Kidhibiti Cha Walimu Wa Kiswahili Katika Kila Shule

| SHULE/KIWANGO | JUMLA |
|---|---|
| A | 8 |
| B | 10 |
| C | 8 |
| D | 8 |
| E | 8 |
| F | 8 |
| G | 8 |
| H | 8 |
| I | 8 |
| J | 8 |
| **JUMLA** | **82** |

(Kiini Mtafiti: 2013)

## 3.7 Ukusanyaji wa Data

Data ilikusanywa kutoka shule za msingi za umma Kisumu Mashariki.Hohaji nanakala za uchunguzi somo zilitumika. Mtafiti alihusisha utafiti wa kitakwimu na wa maelezo katika kuteua visaidizi vya kukusanya data kwa kuzingatia mwongozo waOrodho(2005). Data ilikusanywa nyanjani na maktabani. Nyanjani mtafiti alihoji wanafunzi, walimu na wakuu wa shule. Hojaji zilijazwa kama inavyokusudiwa. Data ilifafanuliwa kwa kusaidiwa na jedwali kwa njia ya asilimia.Utumiaji wa jedwali asilimia, mtafiti alitoa mambo ya muhimu na hitimisho la utafiti.

### 3.7.1 Hojaji

Hojaji ndizo zilikuwa vifaa vikuu katika ukusanyanji wa data.Hojaji hizi zilikuwa za walimu wa kuu ,walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa darasa la tatu.Hojaji hizi zilikaguliwa wakati wa utafiti awali, kurekebisha kasoro zozote ili kudhabiti na kuthamni.

Hojaji hizo zilikuwa na maswali funge na wazi.Walengwa walipata nafsi ya kujieleza vyema bila wasiwasi wowote ule.Hojaji zilitolewa na mtafiti kwa msaada wa walimu wa Kiswahili.Data ya walimu ilisaidiwa na ile ya wanafunzi kupata ukweli wa matumizi ya vifaa katika ufundishaji msamiati wa Kiswahili.

### 3. 7.2 Nakala ya uchunguzi

Mtafiti alitazama somo na kutumia nakala ya uchunguzi kulikagua. Kulingana na aina ya visaidizi vilivyo na umuhimu katika ufunzaji au ufundishaji wa msamiati vilivyotumiwa. Alama (√) au (×) ilitumiwa kujaza sehemu zilizotengwa kuonyesha visaidizi.

### 3.7.3 Mahojiano

Mwalimu mkuu, mwalimu wa Kiswahili na wanafunzi walishughulikiwa kupata data mahususi kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili ili kupata changamoto walizokuwa nazo somo hili katika kuelewa msamiati.

## 3.8 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilipangwa kwa kuzingatia vigezo muhimu na kuiwekwa katika makundi ya msamiati inayolingana ili kuiweka wazi na kuondoa utata. Uwashilishaji datawa kutathmini na kiidadi ulitumika kuchambua vigezo vyote na kubainisha maana na matokeo ya data kwa minajili ya kupata suluhisho na mwishowe kutoa mapendekezo. Data iliwasilishwa kwa kutumia majedwali, grafu na chati. Utafiti awali uliunda chanzo cha kazi hii na utachanganua kazi nzima. Maswali funge na wazi yalichanganuliwa kwa kutumia Statistical Package for Social Sciences (SPSS), hivyo kwa utafiti huu ulidhibitisha kwamba kuna uhusiano wa visaidizi vya ufundishaji na ujifunzaji kuleta uelewekaji msamiati (Kasomo(2007). Kule kusikiliza maoni ya walengwa walipo na, wakati uliotumika. Uadidi ulitumika kueleza wazi mbinu ya uchanganuzi data kwa kina. Vile vile mbinu ya kithamani ambapo kipimo radidi, kipimo cha kati na mini (kipimo cha wastani) vilielezwa kwa kina.

## 3.9 Udhabiti wa Visaidizi

Udhabiti unahusu uhakika na maana ya yale yanayokisiwa ambayo yanategemea matokeo ya utafiti (Orodho 2005). Hivyo basi matokeo hupatikana kwa uchunguzi wa data na swali linalotafitiwa, upimaji wa yale yanayofaa, hupimwa kwa uwakilishaji wa walengwa na uteuzi wa wataalam (Mugenda na Mugenda,1999)

## 3.10 Uthamini

Uthamini wa vipimo, vina viwango na matokeo ya visaidizi vya utafiti vinavyodhibiti matokeo au data inayojirudiarudia baada ya kujaribu. Kuchunguza tengenezi ya kazi hii ili kuhakikisha uthamini utafiti wa awali ulifanyika shule moja ya kaunti ya Kisumu

mashariki.  Mugao nusu ulitumika kulingana na Kothari (1985) unahitaji kujaribu mara moja na hivyo kutupilia mbali kosa au dosari yoyote iliyotokana na maoni tofauti.

### 3.11 Usiri

Mtafiti alizingatia maadili ya hali ya juu. Utafiti huu ulikuwa kwa ajili ya masomo na haukutumika kwa manufaa mengine yoyote. Nilipata idhini kutoka kwa washika dau wa elimu, wakuu wa shule, MOEST na hatimaye walimu wa Kiswahili (Creswell: 2003).

# SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DATA

Katika sura hii mtafiti anajihusisha na uchanganuzi wa data. Katika utafiti huu, Mtafiti alinuia kutathmini kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili katika darasa la Tatu. Wahojiwa wa utafiti huu walikuwa, Mwalimu Mkuu, Walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa darasa la tatu katika shule kumi zilizoko katika Kaunti ya Kisumu Mashariki, Kenya.

## 4.1 Habari za kibinafsi kuhusu wahojiwa

**Mchoro 3: Jinsia ya Walimu Wakuu**




Idadi %

(Kiini Mtafiti: 2013)

Jedwali hili limeonyesha kuwa walimu wakuu 10 walihusika katika utafiti huu, 62.5% walikuwa wanaume wakilinganishwa na 37.5% waliokuwa wanawake.s Matokeo hayo pia yanaonyesha kuwa kati ya walimu wa somo la Kiswahili 10 husika katika utafiti huu, 38.46% walikuwa wanaume wakilinganishwa na 61.54% waliokuwa wanawake ikilinganishwa na wanafunzi ambao 43.9% walikuwa wa kiume huku wenzao wa kike wakiwa 56.1%. Matokeo hayo pia yanaonyesha kuwa Walimu Wakuu walikuwa wamehitimu viwango vifuatavyo vya elimu: 25% walihitu Diploma, 37.5% Shahada ya Elimu, 12.5% Shahada ya Uzamili na 12.5% Shahada ya Uzamifu.Hakuna yeyote (0%) aliyehitimu shahada nyinginezo. Walipoulizwa muda waliokuwa wamehudumu kama

Walimu Wakuu, walijibu ifuatavyo: Hakuna (0%) aliyekuwa amehudumu chini ya miaka 5, 25% walikuwa wamehudumu miaka 5 hadi 10, 37.5% miaka 10 hadi 15, 25.0% miaka 15 hadi 20 nao 12.5% miaka 21 na zaidi. Kuhusu viwango vyao vya elimu, walimu wa somo la Kiswahili walijibu kuwa walikuwa wamehitimu viwango vifwatavyo vya elimu: 23.08% walihitu Diploma, 53.85% Shahada ya Elimu, 15.38% Shahada ya Uzamili na 7.69% shahada nyinginezo. Hakuna (0%) aliyehitimu na shahada ya Uzamifu.

**Mchoro 4: Viwango vya elimu ya walimu wa Kiswahili**




(Kiini Mtafiti: 2013)

Walipoulizwa muda waliokuwa wamehudumu kama walimu wa somo la Kiswahili nao wakajibu ifuatavyo: Hakuna (0%) aliyekuwa amehudumu chini ya miaka 5, 25% walikuwa wamehudumu miaka 5 hadi 10, 37.5% miaka 10 hadi 15, 25.0% miaka 15 hadi 20 nao 12.5% miaka 21 na zaidi. Walimu wa somo la Kiswahili waliulizwa kama walikuwa wakifunza masomo mengine ama ni Kiswahili pekee. Wote (100%) walijibu "Ndio" na wakaorodhesha masomo hayo mengine ifuatavyo: Hisabati 7.69%, Sayansi 23.08%, Social Studies 30.77%, Elimu ya dini 7.69% na mengineyo 30.77%. wote (100%) walijibu kuwa walikuwa wakifunza kati ya wanafunzi 40 na 75 madarasani mwao. Kuhusu masomo mengine waliyofunza mbali na somo la Kiswahili, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: Hisabati 46.15% Kiingereza 38.46%, Sayansi 46.15% Somo la Jamii 30.77%, Elimu ya dini 69.23% na Nyingine 7.69%. Wote (100%) walijibu kuwa walikuwa wakifunza masomo hayo kati. Kulingana na matokeo haya, walimu hao wana

majukumu mengi mno.wanafunzi pia ni wengi mno.kiwango chao cha weledi wa kazi ni wazi kwamba wamehitimu vilivyo na wana umilisi somo. Hata hivyo ni vyema kuboresha ujuzi wao kwa kujiunga na vyuo vya elimu kupata mambo mapya ili kuendeleza mwamko mpya wa elimu. Hili ni jambo nzuri kwa mwalimu yeyote Yule. Kila kuchao kuna hitaji la mwalimu kuwa na uwezo wa kujiboresha ili aweze kupata elimu mpya katika karne hii ya mwamko mpya. Matokeo haya yanawiana na mawazo ya Grove and Hauptfleisch (2008) wanaoeleza jinsi kupata upya wa kufunza na wanafunzi wakaingiliana na visaidizi hivi kuboresha uelewa dhana.Hayo yote ni sawa kwani elimu haina mwisho na kupokea mambo mapya upatapo nafasi ni jambo nzuri.Watu huimbua mambo mapya kila siku hivyo kuna haja ya kuendeleza masomo na kukubali mabadiliko.Huko ndiko kukua na kuendelea mbele badala ya kukataa kujihami na mwamko huo mpya.

## 4.2 Changamoto zilizopo

Walimu Wakuu walijibu kuhusu changamoto zilizopo na majibu yakawa hivi:Katika msamiati wa miti na mimea, 0% waliashiria Kiwango cha juu sana, wakaashiria 50% Kiwango cha juu, 25% wakaashiria Kiwango wastani, 25% wakaashiria Kiwango cha chini wakati ambapo 0% waliashiria Kiwango cha chini sana. Kwenye msamiati wa nyumbani,0% waliashiria Kiwango cha juu sana, 12% 0% wakaashiria Kiwango cha juu, 25% wakaashiria Kiwango wastani, 50% wakaashiria Kiwango cha chini nao 12.5% wakaashiria Kiwango cha chini sana. Hali kadhalika, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo msamiati wa wanyama, 0% waliashiria Kiwango cha juu sana, 37.5% wakaashiria Kiwango cha juu, 25.0% wakaashiria Kiwango wastani, 12.5% wakaashiria Kiwango cha chini nao 25.0% wakaashiria Kiwango cha chini sana. Katika msamiati wa ndege, 0% waliashiria Kiwango cha juu sana, 0% wakaashiria Kiwango cha juu, 12.5% wakaashiria Kiwango cha wastani, 50% wakaashiria Kiwango cha chini na 37.5% wakaashiria Kiwango cha chini sana.

**Jedwali 5: Kiwango cha matumizi ya visaidizi vya ufundishaji na walimu shuleni**

| | 1 | | 2 | | 3 | | 4 | | 5 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | f | % | f | % | f | % | f | % | f | % |
| Msamiati wa wanyama | 0 | 0.0 | 4 | 50 | 2 | 25.0 | 2 | 25.0 | 0 | 0.0 |
| Msamiati wa ndege | 0 | 0.0 | 1 | 12.5 | 2 | 25.0 | 4 | 50.0 | 1 | 12.5 |
| Msamiati wa miti na mimea | 0 | 0.0 | 3 | 37.5 | 2 | 25.0 | 1 | 12.5 | 2 | 25.0 |
| Msamiati wa vyakula | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 1 | 12.5 | 4 | 50.0 | 3 | 37.5 |

(Kiini Mtafiti: 2013)

Nao wanafunzi walipoulizwa iwapo mwalimu wako wa Kiswahili alikuwa akitumia visaidizi vya ufundishaji walijibu hivi:




Mchoro 5: Kiwango cha matumizi ya visaidizi vya ufundishaji na walimu

(Kiini Mtafiti: 2013)

Kwenye Msamiatiwa wanyama, walimu watano(63.49%) walijibu La huku walimu watatu(36.51%)wakijibu Ndiyo. Kwenye msamiati wa ndege,walimu watano(57.14%) walijibu Ndiyo huku,walimu watatu(42.86% ) wakijibu La. Kwenye msamiati wa miti na mimea,walimu watatu(38.1%) walijibu Ndiyo huku ,walimu watano (61.9%) wakijibu La na Kwenye msamiati wa vyakula ,walimu wanne(50.79%) walijibu Ndiyo huku, walimu wane(49.21%) wakijibu La. Walimu wengi hawatumi visaidizi na wakitumia ni kwa

uchache mno hasa picha, ubao na chaki.Vilevile msamiati mingine wao hufunza bila visaidizi vyovyote kama vile msamiati wa miti na mimea,wanyama na ndege wa pori.Hivi ni kusema kwamba wanafunzi hawapewi nafasi mwafaka ya kuingiliana na vifaa hivi, hivyo kutoeleweka kwa dhana jinsi inavyonuiwa kuelewekwa. Visaidizi vimedhibitisha kwamba huwa vinasaidia kuelewa dhana kwa urahisi. Matokeo ya mitihani imeonyesha kwamba ni vyema walimu kuzingatia hayo kwani silibasi inahitaji hivyo katika kila darasa na utaratibu upo.Mfumo wa elimu una mpangilio ambao ni lazima walimu wafuate moja kwa moja ili mwanafunzi afaulu kimaisha.Ni hatia na makosa mwalimu kujua hivyo na akose kutimiza hayo. Pendekezo ni kwamba, washika dau na wahusika wote wa elimu nchini wawe macho na kuhakikisha yote yanatekelezwa. Kulingana na silibasi na mfumo wa elimu ya 8-4-4 msisitizo upo kwamba visaidizi vitumike kufunza madarasa yote.Vifaa hivi vyote vimeorodheshwa vizuri ili walimu waviandae na kuvitumia katika ufunzaji.

Kutokana na matokeo haya, ni wazi kuwa sehemu ambazo visaidizi vimetumiwa ulirahisishwa na kule kuona, kushika na kutazama kwa vifaa hivyo halisi. Mwingiliano wa visaidizi huwapa wanafunzi fursa ya kubuni mambo wenyewe na kuongeza ubunifu basi kukuza vipawa walivyo navyo. Hili jambo husaidia kuweka mambo katika kumbukumbu zao bila kusahau.Mfano wayule anayeendesha baiskeli kila siku na kuwa na uzoefu basi hujifunza kwa kina na kupata ustadi, vivyo hivyo kuna hitaji la mwanafunzi na walimu kuzoea kutumia visaidizi ili kupata uzoefu huo na dhana zikaelewaka vyema. Wanafunzi wanapoona visaidizi hivi kila siku wao hupata uzoefu wakuvitumia msamiati vilivyo kulingana na wale ambao hubuni mambo kwa mbali.Msamiati ukifahamika awali na misingi dhabiti kuwekwa awali ni bora kuliko kurekebisha makosa baadaye. Kulingana na Marine and Hilles (2008) kuona na kutazama kunalete kukumbuka kwa dhana zaidi kuliko kubuni kwa mbali.Visaidizi hivi ndivyo somo kwani unapofunza msamiati wa ndege hakuna haja ya kujaribu kueleza kinyago cha ndege.Itakuwa bora kuwa na mchoro wa ndege huyo na sehemu zake badala yakupoteza wakati na kupata shida kueleza hivyo.Kinyago hicho kitarahihisha somo hilo ili kuleta motisha, kuelewa kwa urahisi,kuweka mambo katika kumbukumbu kuliko kusumbuka kubuni mambo kidhahania.

Wahojiwa walipoulizwa kiwango cha walimu shuleni waliovitumia visaidizi vya ufundishaji darasani, walijibu kama ifuatavyo:

Jedwali 6: Matumizi ya visaidizi madarasani

| | 1 | | 2 | | 3 | | 4 | | 5 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | F | % | f | % | F | % | f | % | f | % |
| Ensiklopidia | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 1 | 12.5 | 7 | 87.5 |
| Majarida | 0 | 0.0 | 2 | 25.0 | 5 | 62.5 | 1 | 12.5 | 0 | 0.0 |
| Magazeti | 0 | 0.0 | 2 | 25.0 | 2 | 25.0 | 3 | 37.5 | 1 | 12.5 |
| Vitabu | 2 | 25.0 | 3 | 37.5 | 3 | 37.5 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |
| Vinyago | 0 | 0.0 | 4 | 50.0 | 3 | 37.5 | 1 | 12.5 | 0 | 0.0 |
| Chati | 3 | 37.5 | 2 | 25.0 | 1 | 12.5 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |
| Ramani | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 1 | 12.5 | 6 | 75.0 | 1 | 12.5 |
| Picha | 4 | 50.0 | 1 | 12.5 | 2 | 25.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |
| Filamu | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 8 | 100.0 |
| Runinga | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 2 | 25.0 | 6 | 75.0 |
| Video | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 1 | 12.5 | 7 | 87.5 |
| Redio | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 1 | 12.5 | 2 | 25.0 | 5 | 62.5 |
| Vinanda/CD | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 2 | 25.0 | 6 | 75.0 |

(Kiini Mtafiti: 2013)

Wanafunzi nao walijibu hivi walipoulizwa kiwango gani mwalimu wake wa Kiswahili alikuwa akitumia visaidizi vya ufundishaji alipokuwa akiwafunza darasani:

**Jedwali 7: Kiwango cha mwalimu wa Kiswahili anavyotumia visaidizi**

| | 1 | | 2 | | 3 | | 4 | | 5 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | F | % | F | % | F | % | F | % | f | % |
| Ensiklopidia | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 29 | 46.03 | 34 | 53.97 |
| Majarida | 0 | 0.0 | 21 | 33.33 | 33 | 52.38 | 9 | 14.29 | 0 | 0.0 |
| Magazeti | 0 | 0.0 | 17 | 26.98 | 16 | 25.40 | 18 | 28.57 | 12 | 19.05 |
| Vitabu | 14 | 22.22 | 21 | 33.33 | 16 | 25.40 | 8 | 12.70 | 4 | 6.35 |
| Vinyago | 0 | 0.0 | 35 | 55.56 | 18 | 28.57 | 10 | 15.87 | 0 | 0.0 |
| Chati | 32 | 50.79 | 21 | 33.33 | 8 | 12.70 | 2 | 3.17 | 0 | 0.0 |
| Ramani | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 34 | 53.97 | 28 | 7.00 | 1 | 1.59 |
| Vinygo | 29 | 46.03 | 24 | 38.10 | 10 | 15.87 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |
| Picha | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 6 | 4.00 | 0 | 0.0 | 57 | 90.48 |
| Filamu | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 7 | 11.11 | 56 | 88.89 |
| Runinga | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 10 | 15.87 | 53 | 84.13 |
| Video | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 9 | 14.29 | 12 | 19.05 | 43 | 68.25 |
| Redio | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 8 | 12.70 | 13 | 20.63 | 42 | 66.67 |
| Vinanda/CD | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |

(Kiini Mtafiti: 2013)

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa kuna utata wa utumizi wa visaidizi vya kufunzia somo la kiswahili hivi msamiati kuuelewa huwa kwa njia ya kidhahania. Jambo hili ni makosa na hatia,kwani silibasi inaorodhesha wazi kwamba kila somo na darasa visaidizi hivi vitumike kama vile vinyago,vibonzo, chati, video, jarida,gazeti na ikiwa walimu watazembea kiswahili hakitawahi kubobea kamwe kwani msamiati wowote ule huwa rahisi ukifunzwa kuwa vifaa hivyo lakini si kidhahania. Ni ombi langu kwamba jambo hili litiliwe maanani mara moja kuboresha kiswahili kama somo lingine lile ili mielekeo hasi ibadilike. Mogeni (2005*)* anasema kuwa mambo yanayoonekana kwa macho huwa kwenye kumbukumbu ya mwanafunzi kwa kipindi kirefu.Ni bayana kuwa wanafunzi wanapoingiliana na visaidizi huelewa na kupata mambo kwa urahisi ikilinganishwa na wale wanao fundishwa bila visaidizi vyovyote. Utekaji hisia katika somo huwezesha uelewa wa dhana vizuri na ni vyema mwelekezi somo ambaye ni mwalimu mhusika atumie visaidizi ambavyo vitahusisha wanafunzi wote. Katika kuona, kushika na kutazama huwa mwanafunzi hawezi kusahau vitu alivyoingiliana navyo. Jambo hili ni muhimu katika kurahisisha uelewa somo. Mwanafunzi hutumia vipawa vyake na kuzidisha kubuni mambo mwenyewe bila kutegemea mwalimu kila wakati.Jambo sasa ambalo linazungumziwa la kuwafanya wanafunzi kuboresha talanta pamoja na vipawa vyao. Walipoulizwa maoni yao kuhusu umuhimu wa kuvitumia visaidizi vya ufundishaji katika somo la Kiswahili, matokeo ya majibu ya wahojiwa yalikuwa kama ifwatavyo:

**Jedwali 8: Maoni kuhusu umuhimu utumiaji visaidizi vya ufundishaji**

| | 1 | | 2 | | 3 | | 4 | | 5 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | F | % | F | % | F | % | F | % | f | % |
| Ensiklopidia | 0 | 0.0 | 4 | 50.0 | 3 | 37.5 | 1 | 12.5 | 0 | 0.0 |
| Majarida | 2 | 25.0 | 5 | 62.5 | 1 | 12.5 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |
| Magazeti | 0 | 0.0 | 3 | 37.5 | 2 | 25.0 | 3 | 37.5 | 0 | 0.0 |
| Vitabu | 8 | 100.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |
| Vinyago | 4 | 50.0 | 2 | 25.0 | 0 | 0.0 | 2 | 25.0 | 0 | 0.0 |
| Chati | 8 | 100.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |
| Ramani | 2 | 25.0 | 3 | 37.5 | 2 | 25.0 | 1 | 12.5 | 0 | 0.0 |
| Picha | 8 | 100.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 |
| Filamu | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 4 | 50.0 | 2 | 25.0 | 2 | 25.0 |
| Runinga | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 2 | 25.0 | 6 | 75.0 |
| Video | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 1 | 12.5 | 7 | 87.5 |
| Redio | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 2 | 25.0 | 3 | 37.5 | 3 | 37.5 |
| Vinanda/CD | 0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 2 | 25.0 | 2 | 25.0 | 4 | 50.0 |

(Kiini Mtafiti: 2013)

Matokeo haya ni thibitisho tosha kuwa ,kunasa hisia za wanafunzi huleta motisha kwa wanafunzi na kuboresha uelewa somo.Ni muhimu kila mwalimu anayejali na mwenye utu kuteka wakati fulani kuandaa somo lake linalonuia kulenga shabaha na kupitisha ujumbe kwa njia rahisi ili kuelewa dhana. Mwalimu kama huyu atapata kazi imerahisisishwa kwa utumizi visaidizi kuliko anayekazana bila vifaa hivyo. Mielekeo hasi kuwa somo ni ngumu yataendelea kukita mizizi ikiwa walimu wa kiswahili hawatambuni njia mpya za kutekeleza hisia za wanafunzi wao. Mtindo mpya wa kufundishia kwa video, vinyago, redio, vinaweza kubadili mawazo kuhusu somo hili na likabadili matokeo ya mitihani.Wanafunzi wataanza kutamani kuzungumza kama wale wanaowatazama katika runinga,kusikiliza katika rediokisha mielekeo hasa kutoka kwa wazazi na walimu.Wanafunzi wakaibadilika hivi kujivunia kiswahili kama lugha ya taifa. Kulingana na Njogu and Nganje (2006) mawasiliano ndiyo njia moja ya miingiliano ya binadamu kokote kule. Wahojawa walipoulizwa kutaja changamoto wanazokumbana nazo wanapotumia visaidizi vya ufundishaji kufunza sehemu za lugha, maoni yafwatayo yaliyotolewana Walimu Wakuu pamoja na Walimu wa Kiswahili na wanafunzi:

(a) Kupata vinyago vya kufunza msamiatiwavyakula huwa tatizo sugu.Vile vile wenye weledi wa kutengeza vinyago huu vigumu.Pesa za kununua chati angalau kuchora huu shida tele.Mazingira vilevile huwa tofauti na kuna yale ambayo ni magumu kuelewa kwa wanafunzi wengine.Hali halisia hueleza mambo vizuri kuliko kueleza msamiati huu. Basi visaidizi vitumike ili uelewa wa dhana uboreke.Hapo awali walimu walienda kuwaonyesha wanafunzi wao mazingira waliomo na kuona,kushika na kuutunza mazingira hayo.Jambo hili sasa limekuwa si la kutiliwa mkazo na wanafunzi hupata masomo yote mle darasani eti matokeo ya mtihani.Wakati huo wanafunzi hawapati kuingiliana na mazingira angalau wapate kujifunza mawili matatu kutoka kwa mazingira basi tuendako ni kuelimisha wanafunzi ambao hawajiwezi kwa mambo mengi ila kufanya mitihani.Ulimwenguni kwote elimu inafaa humwezesha mwanafunzi kuzuwa mambo mwenyewe,kuingiliana na hali halisia ili awe na uwezo wa kusuluhisha changamoto atakazo kumbana nazo maishani.Jambo hili likifanyika utata wa kazi utatatuliwa kwani wanafunzi watakuza vipawa vyao jinsi inatakikana.

(b) Msamiatiwa wanyama wa pori huwa una utata hata kwa walimu. Majina ya wanyama huwa ni rahisi kwa wanafunzi kwa lugha ya kiingereza ilhali huwa mgumu katika Kiswahili.Swali kuu ni kwamba wanafunzi huingilianana msamiati huu wa kiingereza kila wakati hivyo kuwa na mazoea, vivyo hivyo kwa walimu wa Kiswahili tuwape wanafunzi nafasi ya kuingiliana na msamiati huu kila mara ili wawe na uzoefu huo. Mazingira huwa pengine hayaruhusu kuiingiliana na huo msamiati.Pesa za kuwapeleka wanafunzi kuzuru sehemu hizo ili waweze kutambua msamiati huo kwa urahisi hamna.Wakuu wa shule vilevile hupata senti kidogo za kununua vitabu hivyo kukosa pesa za kugharamia vifaa shuleni.Warsha za kusaidia walimu walio na udhaifu wakubuni vifaa vya kufunzia zitasaidia sana ili motisha ya somo la Kiswahili uboreshwe na kubadili maoni kwamba somo hili ni gumu na ni la watu wa hadhi ya chini. Mielekeo hasi itabadilika kwa walimu wa Kiswahili, wanafunzi na wazazi kwa jumla.

(c) Msamiatiwa ndege wa pori huwapa walimu na wanafunzi ugumu mkubwa. Wakati mwingi walimu upuzilia mbali kuelekeza wanafunzi sababu hawawezi kulinganisha majina ya kiingereza na Kiswahili ya ndege pori hivyo huwapa wanafunzi zoezi la kuchora bila kuwaeleza. Wengine walimu huhepa kulifunza somo hili,hivi kuwadhulumu wanafunzi kwani dhana hizi hutahiniwa kwingineko. Ni dhahiri kuwa msamiati huu ukitahiniwa katika darasa la nane wanafunzi huona kwamba hawajawahi kuiingiliana nao hata kidogo kwani walimu huupuzilia mbali katika darasa la tatu.Jambo hili si geni kwani katika maiingiliano ya walimu na wanafunzi ni wazi kwamba msamiati hutumika vibaya. Mfano mavazi fulani kama suruali huchukuliwa kama ni mamoja na chupi, long'i na kaptura.Vyakula kama pojo na ndengu hadi sasa yanafahamika vibaya,hoho na pilipili mboga hazieleweki na wengi hata walimu hufunza kimakosa hadi leo.Huko sokoni,wateja na wanunuzi hutumia msamiati kimakosa.Jambo hili la weza kubadilishwa na walimu wa Kiswahili wanapotumia visaidizi hivi ili wanafunzi waiingiliane na dhana kutoka mwanzo wa kuweka misingi katika darasa la kwanza hadi darasa la nane na kuendelea. Kiswahili kitatia fora na kubadilisha mielekeo hasi.Somo hili litapendeka na wote kwani kuna mabadiliko mapya ya kujifunza na dhana kueleweka kwa urahisi kama masomo mengine.

(d) Msamiati ya mimea na miti huleta changamoto kubwa kwani walimu kwa wanafunzi huwa mazingira yao hayana miti au mimea hiyo. Visaidizi vya msamiati hii huwa migumu sana kupata naikipatikana huwa changamoto kulinganisha na hali halisia. Mazingira waliomo walimu na wanafunzi huzuia uelewa wa somo vizuri na kuzuru sehemu fulani ingawa jambo hili halifanyiki sana. Ni vyema walimu wakuu kuwacha huru jambo la kupanga na kuweka fedha fulani za kutalii sehemu kadhaa kulingana na mahitaji ya somo.Wazazi vilevile watoe mchango wao kuelekeza na kuwasaidia wanao kutambua misamiati tofauti tofauti wanapozuru sehemu kadhaa wakati wa likizo kama vile porini,mashambani,mijini na mahali pa kuabudu.

## 4.3 Sera za kudhibiti matumizi mwafaka ya visaidizi

Walimu Wakuu pamoja na Walimu wa Kiswahili waliulizwa iwapo shule zao zilikuwa na sera ya kudhibiti matumizi mwafaka ya visaidizi madarasani na matokeo ya majibu yao yalikuwa hivi:

**Jedwali 9: Sera ya kudhibiti matumizi mwafaka ya visaidizi madarasani**

| | Ndiyo | | La | |
|---|---|---|---|---|
| | f | % | f | % |
| Msamiati wa wanyama | 3 | 37.5 | 5 | 62.5 |
| Miti na mimea | 0 | 0.0 | 8 | 100.0 |
| Msamiati wa vyakula | 5 | 62.5 | 3 | 37.5 |
| Msamiati wa ndege | 0 | 0.0 | 4 | 50.0 |

(Kiini Mtafiti: 2013)

Katika Msamiati wa wanyama, 62.5% walichagua La nao 37.5% wakachagua Ndiyo. Katika miti na mimea, wote (100.0%) walichagua La. Katika msamiati wa vyakula, 37.5% walichagua La nao 62.5% wakachagua Ndiyo. Katika msamiati wa ndege, 50.0% walichagua La,nao 50.0% wakachagua Ndiyo. Walieleza sababu zao kuchagua majibu hayo ifuatavyo:Ni wazi kwamba sehemu fulani hazishughulikiwi na wakati mwingine zinahepwa. Silibasi inaeleza wazi jambo hili kwa hivyo litekelezwe. Mitihani ya kitaifa imeonyesha jambo hili wazi kwani wakitahini vipengele vya madarasa ya chini matokeo huwa duni hadi walimu wanalalamika jinsi mtihani ulivyomgumu eti vipengele vile havimo katika silabasi. Huu ni mwamko mpya na lazima walimu wajihami na silibasi wajue mahitaji ya kila darasa ni yapi na watawasilisha ujumbe vipi ueleweke kwa urahisi. Silibasi imeorodhesha vifaa vyote vya kila darasa na hivyo walimu wasipuuzilie hayo. Kuhusu sera iliyokuwa shuleni mwao ya kubuni visaidizi vya kufundisha sehemu teule za lugha ya Kiswahili, Walimu Wakuu,Walimu wa Kiswahili na wanafunzi walijibu hivi:

(a) Silibasi inahimiza utumiaji wa viasidizi katika kufunza msamiati wa vyakula.Sera hasa ya shule kutengeneza hamnalakini kila mwalimu anahimizwa kuunda vifaa hivyo. Changamoto vilevile zinazidi kutokana na wingi wa wanafunzi, sehemu za kuhifadhi,fedha za kununua visaidizi.

(b) Msamiatiwa wanyama wapori hamna.Wanapofikiria kuzuru sehemu mbalimbali huwa ni katika somo la jiografia.Walimu hawafikirii kutumia wakati huo kuelimisha wanafunzi msamiati wa wanyama ingawa wengine pia wana shida ya utambuzi huo.

(c) Msamiatiwa ndege wa pori haushughulikiwi wakati jopo hujadili haya. Cha muhimu huwa matokeo bora ambayo ndiyo kiinua mgogo wa shule zote bila kukumbuka kwamba matokeo borahuanzia kwenye ufundishaji mwema.

(d) Hamna sera za kuunda vifaa vya kufunzia. Jopo huwa inajadili mambo ya utengezaji ratiba, maandalizi somo na pengine matokea ya mtihani bila kujali vipi somo hufundishwa.

Walimu Wakuu pamoja na Walimu wa Kiswahili na wanafunzi walipoulizwa iwapo shule ilikuwa na sera ya kutoa ukaguzi wa muchanganuzi ya visaidizi vya ufundishaji wa sehemu mbalimbali za lugha madarasani, 37.5% walichagua Ndiyo nao 62.5% wakachagua La na wakaeleza sababu za kuchagua majibu yao ifuatavyo:Jopo huwa halina mtindo huo pengine kuwa na wakaguzi kutoka idara ya elimu,walimu wakuu ambao hukagua walimu wa kiswahili. Walimu wengi walipoulizwa jambo hili walieleza kuwa kupata vifaa hivi huwa shida. Kuhusu kiwango cha mapato ya shule yaliyotumika kununulia visaidizi vya ufundishaji wa sehemu mbalimbali za lugha, Walimu Wakuu pamoja na Walimu wa Kiswahili waliashiria matokeo haya: 5.56% asilimia 5 au chini, 27.78% asilimia 5 hadi 16.67% asilimia 21 hadi 25, 22.22% asilimia 26 hadi 30 na 27.78% asilimia 31 au zaidi.

Mchoro 6: Kiasi cha mapato yanayotumiwa kununulia visaidizi




(Kiini Mtafiti: 2013)

Kuhusu swali iwapo walimu walipata warsha za kuboresha ubunifu wa matayarisho ya visaidizi vya ufundishaji wa sehemu mbalimbali za lugha, Mwalimu mkuu pamoja na Walimu wa Kiswahili wote (100%) walijibu La na kueleza sababu ya kuchagua majibu yao hivi:Kudhibitisha hayo washika dau wa elimu huzuru shule kadhaa tu ambapo nia yao ni kuchunguza mwalimu anavyofunza.Wakati mwingi wao huangalia ratiba, maandalizi somo, usafi, idadi ya wanafunzi na matokeo ya mtihani wa kitaifa. Warsha vilevile huelekezwa kwenye mbinu za uandishi insha au vitabu ambavyo vinatumika kufunzia, vitabu vya kiada. Warsha za kuunda visaidizi au za kuboresha jopo katika kubuni sera za kuunda vifaa hivi vya kufunza havijabobea. Ni jambo la kujadiliwa kwani walimu wa kiswahili hawafanyi hivi.Ni vyema kila shule ibuni jopo la kuangalia matumizi ya visaidizi,utengenezaji na kuhakiki kuona kwamba uzoefu wa kutumia visaidizi hivi umetia fora na kutumika wakati wote ili kusaidia uelewa dhana kwani kutumia mara moja ni kama kutotumia kabisa.

Wahojiwa walipoulizwa iwapo kulikuwa na mikakati ambayo iliwekwa kuzingatia mahudhurio katika warsha za kuboresha ubunifu, 62.5% walijibu Ndiyo nao 37.5% wakajibu La. Walitoa sababu zifuatazo kuelezea sababu za kuchagua majibu yao. Walipoulizwa iwapo walimu wa somo la Kiswahili huwa na vikao vya kujadili uchanganuzi wavisaidizi vya ufundishaji wa sehemu mbalimbali za lugha katika

masomo, Walimu Wakuu pamoja na Walimu wa Kiswahili wote (100%) walijibu La na na kueleza sababu ya kuchagua majibu yao hivi:Wakati uchanganuzi unafanyika huwa wa vipengele kama matokeo ya mitihani,utaratibu wa kufunza,ratiba na maandalizi ya somo. Sera ya kuchanganua utumizi wa visaidizi haupo katika Kaunti hii ya Kisumu. Walimu Wakuu, Walimu wa Kiswahili na wanafunzi wote (100%) walijibu Ndiyo walipoulizwa iwapo walidhani kuwa matumizi ya visaidizi vya ufundishaji wa misamiati ya somo la Kiswahili uliathiri matokeo ya mtihani. Walitoa sababu zifuatazo kuelezea sababu za kuchagua majibu yao:Msamiati hutatiza wanafunzi sana wanapoulizwa kujieleza kwa lugha hii.Wengi wao husema kwamba hawajui mambo fulani katika lugha ya kiswahili hivyo utata katika kutumia kwa mfululizo.Mfano wanafunzi ambao hufanya vizuri katika mitihani yao ya kitaifa huo wanashida ya kujieleza vizuri.Miingiliano ya mawasiliano hayo huwa na shida kwa kiwango kikubwa tu. Shida hii imezua utata wa kukosekana wahutubi, wasomaji habari naweledi katika kujieleza vyema katika hadhara fulani kama ilivyo katika kiingereza.Kulingana na Su and Hong (2007), utumiaji wa visaidizi husaidia pakubwa mno.

## 4.4 Udhaifu au ufaafu wa matumizi ya visaidizi vya ufundishaji

Walimu Wakuu pamoja nawalimu wa Kiswahili waliulizwa kutaja mbinu zilizokuwa mwafaka za kutumia visaidizi vya ufundishaji wa sehemu mbalimbali za lugha nao wakajibu hivi:

(a) Kufundisha msamiati wa vyakula ukitumia visaidizi huleta motisha,kunasa hisia za wanafunzi.Dhana hii hupendeza wanafunzi, huwafanya wao kulinganisha yale wajuayo nayale ambayo ni mageni kwao. Wakati mwingine msamiati huuhuu hujulikana kwa lugha ya mtaa au kiingereza ambapo si Kiswahili mwafaka.Kutia misingi mwafaka ni vyema kuliko kurekebisha makosa yaliyofanyika awali.

(b) Msamiatiwa wanyamawapori na mazingira huwa tofauti kabisa na ni vyema kutumia vinyago, filamu, video au kuzuru sehemu hizi. Jambo hili ni gumu kwa shule nyingi kwa sababu ya changamoto zilizozungumziwa awali.Ufundishaji huwa kazi rahisi ikiwa mwelekezi amejianda vizuri. Katika somo kama hili

mwalimu hubadilika kuwa mwelekezi na mwanafunzi kuhupata nafasi ya kuingiliana na visaidizi hivi. Vipawa hukuzwa, ubunifu pia hujengwa na kutoa nafsi ya wanafunzi kugundua mambo wenyewe. Jambo hili na mwigiliano wa wanafunzi na visaidizi huboresha kukumbuka kwa dhana walizofunzwa. Matokeo ya mitihani yatabadilika na mielekeo hasi itabadilika.

(c) Vifaa vikitumika kufunza msamiati wa ndege wa pori ni kweli shida ipo na kuufunza msamiati huu na njia ndege wa porini dhana hueleweka kwa urahisi.Mvuto wa somo utabadili mielekeo hasina hivyo kubadili dhana kwamba Kiswahili ni kigumu. Uzoefu huleta tabia ya kuvutia hisia na kurudiarudia hivyo hurahisisha ugumu wa mambo yaliyofahamika kuwa magumu. Walimu Wakuu pamoja na Walimu wa Kiswahili waliulizwa kutaja nani shuleni aliyetoa uamuzi kuhusu ununuzi au utayarishaji wa visaidizi vya ufundishaji vinavyotumika madarasani, nao wakajibu ifuatavyo: 75% ya Walimu Wakuu walijibu ni Mwalimu Mkuu, 25% walijibuni Naibu Mwalimu Mkuu, 50% walijibu Jopo la walimu wa somo, 25% walijibu Mwalimu wa somo binafsi na 37.5% wakajibu Walimu wa somo la Kiswahili kwa pamoja. Walimu wa Kiswahili nao walitoa majibu yao hivi: 69.23 walijibu Mwalimu Mkuu, 46.15 wakajibu Naibu Mwalimu Mkuu, 38.46% wakajibu Jopo la walimu wa somo, 46.15% wakajibu Mwalimu wa somo binafsi naye 30.77% wakajibu Walimu wa somo la Kiswahili kwa pamoja.

**Jedwali 10: Wenye uamuzi kuhusu ununuzi au utayarishaji wa visaidizi**

| | Walimu Wakuu | | Walimu wa Kiswahili | |
|---|---|---|---|---|
| | f | % | F | % |
| Mwalimu Mkuu | 6 | 75.00 | 9 | 69.23 |
| Naibu Mwalimu Mkuu | 2 | 25.00 | 6 | 46.15 |
| Jopo la walimu wa somo | 4 | 50.00 | 5 | 38.46 |
| Mwalimu wa somo binafsi | 2 | 25.00 | 6 | 46.15 |
| Walimu wa somo kwa pamoja | 3 | 37.50 | 4 | 30.77 |
| | N = 8 | | N = 13 | |

(Kiini Mtafiti: 2013)

Jedwali hili linathibitisha kwamba walimu wakuu ndiyo waamuzi wa ununuziwa visaidizi vyote vinavyonunuliwa shuleni. Ingawa walimu wa somo ndio wahusika na maadalizi ya

